SUPA JACKPOT
TZS.1,051,207,683
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**RIPOTI MAALUM**
Halmashauri ilivyo hatarini kugeuka jangwa




UKURASA 13


# Nipashe

Jumamosi Novemba 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581134

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## ZITTO KABWE

# Ashtuka ukimya utekelezaji hoja za Kikosi Kazi

**MJADALA** uteuzi wa Dk. Mwinyi waibua vigogo CCM...*Endelea Uk. 2*



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, SACP Ramadhani Ng'anzi (kulia), akitoa elimu kwa askari wake, kuhusu mfumo mpya wa kamera za kubaini makosa ya madereva, kama kuongea na simu, kuendesha mwendokasi na makosa mengine ya usalama barabarani, wakati wakiufanyia majaribio mfumo huo, eneo la Msembeta, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhi cheti cha udhamini wa Tuzo za 16 za Rais za wazalishaji bora wa viwandani (PMAYA), kwa Mkurugezi Mtendaji wa kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, Raman Ananthanarayanan, katika hafla iliyoandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), jijini Dar es Salaam jana. Bonite iliibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Mzalishaji Bora wa vinywaji visivyo na kilevi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bonite mzalishaji bora wa vinywaji

UKURASA 3

# Utata kifo mfanyabiashara akiwa na mkewe nyumbani

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, RUVU MECHI DUME** UK. 32 **KATUNI** UK. 6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza katika mkutano wa Mabalozi wa Tanzania wanaowakilisha Tanzania Nje ya Nchi, wilayani Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Zitto ashtuka ukimya hoja za Kikosi Kazi

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe ameitaka serikali itoe ratiba ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi hatua kwa hatua ili itakapofika mwezi Juni mwakani iwe na sheria mpya ya vyama vya siasa, sheria mpya ya uchaguzi na marekebisho ya sheria ya mchakato wa katiba mpya.

Mbali na kutaka ratiba ya utekelezaji wa mapendekezo hayo, kiongozi huyo pia amezitaka asasi za kiraia na vyama vya kijamii kutoa shinikizo kwa serikali kuchukua hatua stahiki ili kuleta mageuzi nchini.

Zitto alitoa kauli hiyo jana wilayani Ruangwa, Mkoa wa Lindi akiwa katika ziara ya chama hicho yenye lengo la ujenzi na kusikiliza kero mbalimbali za wananchi

Alisema tangu ripoti ya Kikosi Kazi ikamilike, hakuna hatua zozote za utekelezaji, huku akiitaka Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inashughulikia masuala ya sera na sheria za uchaguzi, kuanza kufanyia kazi mapendekezo ya taarifa ya Kikosi Kazi.

"Tunapata wasiwasi mkubwa sana juu ya hatua za utekelezaji. Mfano, kwa utaratibu wa kawaida wa kiserikali ilitarajiwa kwenye Mkutano wa Bunge uliopita taarifa ya Kikosi Kazi kuwasilishwa bungeni kama hati ya kuwasilishwa mezani ili kutoa nafasi ya kila mbunge kupitia taarifa hiyo, lakini haikufanyika," alisema Zitto.

Aliongeza kuwa ni wakati mwafaka sasa wadau mbalimbali kupitia majukwaa ya kisiasa kama vile Baraza la Vyama vya Siasa na Kituo cha Demokrasia nchini kuanza mijadala katika ngazi ya mikoa na wilaya kuhusu mapendekezo ya kisheria ili kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaokuja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 unakuwa huru na haki.

Zitto alisema ACT Wazalendo iliamua kuongoza umma ili kuhakikisha taifa linafanya mageuzi ya kidemokrasia na uendeshaji wa siasa sahihi tokea awali kwa kukubali kuingia kwenye mijadala ya aina yoyote ambayo ingeweza kuwa na mchango wa kubadilisha siasa na kutoa ushirikiano kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwenye azma ya kufanya mageuzi ya kisiasa nchini.

"Hatukufanya hivyo kibubusa au kujisalimisha bali kutokana na tafakuri ya kina juu ya hali ya kisiasa kwa sasa ambayo tuliona inatoa mwanga wa matumaini kwamba tunaweza kusukuma mabadiliko ya kisiasa.

"Mathalani, kuwapo kwa fursa ya kukaa meza moja kujadiliana na Rais. Pili, kauli za Rais mwenyewe kuvitaka vyama kuwa na mwanzo mpya kwa kukutana na vyama vya upinzani kujadiliana," alisema.

Zitto alisema ACT iliona fursa hiyo na kuchukua hatua kadhaa za kusukuma mabadiliko ya kisheria ili kurejesha siasa kwenye hali yake ya kawaida badala ya kutegemea utashi wa watawala.

Alizitaja hatua walizochukua kama chama ni pamoja na kushiriki vikao vya pamoja vya wadau wa siasa nchini ukiwamo Mkutano wa Wadau wa Siasa uliofanyika Desemba mwaka jana ambao uliochangia kuundwa kwa Kikosi Kazi.

Akizungumzia hali ya wananchi wa Ruangwa, Zitto alisema kilio chao kikubwa ni sawa na cha wakazi wa maeneo mengine ya kusini - kushuka kwa bei ya korosho kutokana na ukubwa wa kodi unaochukuliwa na serikali.

Awali akiwa katika Kata za Luchelegwa, Nangumbu, Narungombu na Ruangwa kwa ajili ya kufungua matawi ya chama hicho, Zitto alielezwa na wananchi kuwa kilio chao kikubwa ni kukosekana kwa bei nzuri ya korosho pamoja kukosa huduma bora ya maji.

**VIGOGO CCM**

Wakati Zitto akihoji ukimya huo, Waziri wa zamani katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Haji Omar Kheir na mwanasiasa mkongwe, Baraka Mohamed Shamte wameibuka na kusema uteuzi unaofanywa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi haupaswi kuhojiwa na yeyote.

Wanasiasa hao wametoa kauli hiyo ikiwa ni siku chache baada ya ACT Wazalendo kukosoa uteuzi wa mmoja wa viongozi wa Tume ya Uchaguzi (ZEC).

Kwa nyakati tofauti kisiwani Unguja jana, vigogo hao kila mmoja alidai kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud ni mshauri na wala si mbia wa Rais na hana mamlaka ya kupinga uamuzi wa Rais.

Kher alidai kitendo cha viongozi wa ACT Wazalendo kutoa matamshi ya kupinga uteuzi uliofanywa na Rais Mwinyi wa Mkurugenzi wa ZEC, kinaonyesha utovu wa nidhamu, kukiuka misingi ya utawala bora na kutojua mgawanyo wa madaraka.

Kheir alisema kuwa kama uteuzi uliofanywa na Rais umefanyika kisheria na kutangazwa, hakuna anayeweza kuhoji au kukosoa ikiwa sheria na kanuni zilizopo zimezingatiwa.

Alisema pamoja na kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais anatajwa na Katiba ya Zanzibar kuwa mshauri namba moja wa Rais, Rais wa ana hiari ya kuchukua ushauri toka kwake au kukataa.

"Mtu kuwa mshauri hawi na nguvu za kukwamisha uamuzi au kumpinga aliyekuteua na kubatilisha alichoamua. Kwa kawaida mshauri au waziri mwenye dhamana anapotofautina na msimamo wa Rais, hujiondoa kiungwana serikalini," alisema Kheir.

Naye Shamte akizungumza akiwa nyumbani kwake Mkunazini, Zanzibar jana, alisema Makamu wa Kwanza wa Rais, iwe ameshauriwa au la, hana uwezo wa kumhoji bosi wake (Rais) au kumpinga kwa namna yoyote.

Shamte alisema kazi ya usaidizi mara nyingi anayesaidia kazi yake ni kupeleka mawazo, fikra na ushauri lakini uamuzi utaendelea kubaki kwa mwenye nguvu za kisheria ambaye ana haki ya kukubali au kukataa.

Alisema Dk. Mwinyi kwa wakati huu ndiye Rais wa Zanzibar, hivyo haifai anapofanya uamuzi wake upingwe kwa shinikizo la chama cha siasa chochote.

"Nimewasikia viongozi wa ACT Wazalendo wakimshutumu Rais Dk. Mwinyi kumteua Faina kuwa Mkurugenzi wa ZEC. Madai yao kwamba mwaka 2020 uchaguzi ulivurugwa Zanzibar. Hata Hayati Maalim Seif alikubali matokeo na kuapishwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais," alisema.

Mwanasiasa huyo ambaye hivi karibuni alitekwa na watu wasiojulikana, alisema kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hakutoi tafsiri kwamba kila mpinzani au anayetoka chama tawala awe na haki ya kuhoji au kupinga uamuzi wa Rais.

## Utata kifo mfanyabiashara akiwa na mkewe nyumbani

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MFANYABIASHARA Hassan Mbaruku, Mkazi wa Songe, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, amepoteza maisha katika mazingira yenye utata, baada ya kudaiwa kuchomwa kisu akiwa na mkewe nyumbani kwake.

Mbaruku alifariki dunia juzi usiku wa manane akiwa anatibiwa katika Hospitali Teule ya Wilaya hiyo, inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki.

Akizungumzia mauaji hayo kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Henry Mwaibambe, alikiri kupokea taarifa za mauaji hayo, huku akiahidi kutoa taarifa kuhusu uchunguzi wa awali baada ya kufika eneo la tukio.

"Ni kweli hilo tukio lilitokea jana (juzi) na hivi sasa niko njiani naelekea huko. Nitatoa taarifa rasmi baada ya kuona, tutawasiliana. Lakini hakuchinjwa kama inavyoelezwa bali alichomwa kisu," alisema.

Kwa mujibu wa msemaji wa familia ya Mbaruku, Bakari Malamula, kabla ya kupoteza maisha, alitembea kwa mguu mwenyewe hadi hospitali ya wilaya kutafuta tiba.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, daktari wa zamu aliyempokea mgonjwa huyo hospitalini kabla kufariki dunia, Dk. Frank Kasonzo, alisema walimpokea Mbaruku majira ya saa 9.00 alfajiri akiwa amechomwa kisu upande wa kulia kwenye shavu.

"Tukajaribu kulivuta kwa mikono ya kawaida ikashindikana lakini ikabidi tuongeze njia na kufanikiwa kukitoa" alisema. Dk. Kasonzo.

"Nachoweza kusema ni kwamba kifo cha marehemu kilisababishwa na kushindwa kupumua kutokana na koo kuziba kwa sababu ya kuvimba kwa ulimi," aliongeza.

## HABARI KITAIFA

# HakiRasimali yamulika uwajibikaji sekta uziduaji

**Na Halfan Chusi**

HAKIRASILIMALI, mtandao wa mashirika 17 yanayotetea masuala muhimu na ya kimkakati katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia, imewaalika wadau kushiriki Jukwaa la Uziduaji linalolenga kushawishi uundaji wa sheria na sera bora, usimamizi bora wa mapato ya sekta ya uziduaji na kuhamasisha sauti za jamii katika kujihusisha na michakato ya sekta ya uziduaji.

Jukwaa hilo mwaka huu limepangwa kufanyika jijini Dodoma kwa siku mbili kuanzia Novemba 24 mwaka huu kwa lengo la kuwaleta pamoja wadau katika sekta ya uziduaji kwa ngazi zote kujadili kwa kina, kubadilishana uzoefu na kujifunza ili kuendeleza uwazi na uwajibikaji katika sekta ya uziduaji na kuunda mifumo endelevu ya ukuaji wa sekta unaochagizwa na asasi za kiraia.

"Yote haya ni katika juhudi za kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Mkutano huu unatarajiwa kuhudhuriwa na Wizara ya Madini na taasisi zake, Wizara ya Nishati na taasisi zake, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ardhi, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, Kampuni za Uziduaji, Washirika wa Maendeleo, balozi mbalimbali, Asasi za Kiraia (AZAKI), mashirika ya jamii na mashirika ya dini," alisema Adam Antony, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi.

Alizitaja mada za jukwaa hilo zitajumuisha: Uwazi na uwajibikaji katika sekta ya uziduaji; ushiriki wa nchi wanachama katika mchakato wa kimataifa wa Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Uziduaji; utawala wa kudumu na uwekezaji na jinsi Tanzania inavyoweza kuboresha ukusanyaji wa mapato ya serikali na kuvutia uwekezaji katika sekta ya uziduaji.

Zingine ni madini ya kimkakati na mchango wake katika nishati nchini; matatizo ya jamii katika sekta ya uziduaji: haki za binadamu na utatuzi wa matatizo pamoja na siasa za kimataifa katika sekta ya uziduaji.

"Shirika linaamini kwenye uwazi na uwajibikaji wa sekta ya uziduaji kwa ustawi wa watanzania wote," mkurugenzi huyo alisema.

# Bonite yatwaa tuzo uzalishaji bora vinywaji



Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kulia), akikabidhi Tuzo ya Mzalishaji Bora wa vinywaji visivyo na kilevi, kwa Mkurugezi Mtendaji wa kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, Raman Ananthanarayanan (katikati), wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za 16 za Rais za wazalishaji bora wa viwandani (PMAYA), zilizoandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa Maji ya Kilimanjaro, Shafi Rahman. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Bonite Bottlers inayotengeneza soda jamii ya Coca Cola na maji ya Kilimanjaro, imeibuka mshindi katika Tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora wa mwaka 2021 katika kundi la wazalishaji wa vinywaji baridi.

Wakati Bonite ikibuka kinara katika kundi hilo, Kampuni ya Saruji Tanga, imeibuka mshindi wa jumla katika tuzo hizo zilizoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania.

Katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo ambazo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, kampuni ya Kilimanjaro Cable ilishika nafasi ya pili kwa ushindi wa jumla huku Ando Roofing ikiwa ya tatu.

Kabla ya kutolewa tuzo hizo, wafanyabiashara na wawekezaji walitoa hoja mbalimbali ambazo ni vikwazo kwao katika ufanyaji biashara, hali ambayo ilimlazimu Dk. Mpango kujibu na kutoa maagizo katika kuzitatua.

Dk. Mpango katika kutoa mwanga wa utatuzi huo, alivitaka vyombo vya dola na mamlaka za serikali kushughulikia vikwazo na mambo yanayokwamisha uwekezaji nchini ikiwamo bidhaa za magendo, tozo za stempu za kielektroniki, msongamano wa mizigo bandarini na 'blue print'. Kuhusu bidhaa za magendo, Dk. Mpango aliviagiza vyombo vyote vinavyohusika vikiwamo vya dola kulishughulikia kwa haraka suala hilo.

"Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam (Amos Makalla) umekuwa kinara wa usafi Dar es Salaam. Baadhi ya njia za panya ziko katika mkoa wako nina uhakika utafagia bidhaa za magendo zote na wakuu wa mikoa yote nchini, lazima vyombo visaidie kudhibiti biashara za magendo," aliagiza. Kiongozi huyo pia alisema bado bidhaa ghafi nyingi zinauzwa nje ya nchi na kusababisha nchi kupata fedha kidogo na kukwamisha ajira za vijana wa Kitanzania.

Kuhusu tozo za stempu za kielektroniki hasa kwa bidhaa za ushuru, Dk. Mpango aliwahakikishia wanachama wa CTI kuwa serikali inalifanyia kazi na taasisi husika na serikali itawashirikisha wadau na suluhu itapatikana hivi karibuni na itatolewa kwa gharama ndogo.

Dk. Mpango aliitaka Wizara ya Uwekezaji kuharakisha blue print ambayo wadau wanaitaka.

Dk. Mpango pia aliiagiza wizara husika pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kulifanyia kazi ndani ya wiki mbili na taarifa yake iwasilishwe kwa Waziri Mkuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alisema madhumuni ya tuzo hizo ni kutathmini na kuenzi umuhimu wa mchango wa viwanda katika uchumi wa nchi, kutoa fursa kwa wadau kukutana na kutumia fursa za uongezaji wa uzalishaji viwandani.

Alisema tuzo hizo zilianza kutolewa tangu mwaka 2005 zikadorora wakati wa janga la UVIKO-19, na washindi hupatikana kwa vigezo ambavyo baadhi ni ufanisi katika uzalishaji , mauzo ya nje na uingizaji wa fedha za nje, uzalishaji kwa kutumia teknolojia katika viwanda, matumizi bora ya nishati, utunzaji wa mazingira na afya na uwiano wa kijinsia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, ambao ni wadhamini wakuu wa tuzo hizo, alisema zinalenga kutambua mchango wa sekta ya viwanda na kuchagiza uchumi wa taifa.

# Bosi trafiki aanza na magari ya vimulimuli

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng'anzi, amewaagiza makamanda wa vikosi vya usalama barabarani (RTO) kuyakamata magari yote yanayotumia vumulimuli bila vibali.

Pia ameagiza wakuu hao wa usalama barabarani kuwakamata madereva wa bodaboda wote wasio na kofia ngumu.

Ng'anzi alitoa maagizo hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akifanya majaribio ya kamera za usalama barabarani zenye mfumo wa kutambua makosa yanayofanywa na madereva wakati wa kuendesha magari.

"Kuanzia leo (jana) natoa saa 24 kwa magari yote yaliyofungwa vimulimuli na ving'ora kinyume cha sheria watoe. Nawaagiza wakuu wa usalama barabarani wa mikoa nchini baada ya muda huo, wakiona magari hayo wang'oe na wawaandikie faini" alisema.

Alisema kisheria yako magari ambayo yanaruhusiwa kufunga alama za kuonyesha udharura barabarani ambayo ni ya polisi, zimamoto na wagonjwa.

Pia alisema majaribio hayo ya mifumo ya udhibiti wa ajali nchini ni ya pili baada ya kufanyika mkoani Dar es Salaam .

Licha ya sheria zilizopo, alisema bado kuna ajali zinatokea na baada ya utafiti uliofanyika, wameshirikiana na kampuni ya Vitronic ambayo imekuja na teknolojia ya kudhibiti makosa ya usalama barabarani.

Mfumo huo utakuwa unapima mwendokasi, ulevi, madereva wanaotumia simu wakati wa kuendesha na madereva ambao hawajafunga mikanda na wanaoyavuka magari mengine bila kufuata sheria.

Kamanda Ng'anzi alisema mfumo huo ukifanikiwa, utabadilisha tabia za madereva wanapokuwa barabarani ili kuzuia ajali. Kipindi cha kuelekea mwishoni mwa mwaka, alisema jeshi hilo limejipanga kwa kuweka vipima ulevi kila sehemu ili kuhakikisha muda huo wote kunakuwa hakuna ajali.

Aliwaonya madereva wa serikali na taasisi zake kufuata sheria za usalama barabarani kwa sababu wao ndio waliopewa leseni za udereva si viongozi wanaowaendesha, hivyo wakivunja sheria, wataadhibiwa.

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa kampuni ya Vitronic, Abdelhalim Kamal, alisema kampuni hiyo yenye makao makuu yake nchini Uingereza, inafanya kazi kwenye nchi mbalimbali duniani


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
18.11.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 21-11-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 464 DYG / T 837 DYG T 468 DYG / T 887 DJB T 402 DFE / T 394 DVS / T 645 DFA / T 387 DHQ T 305 CZS / T 777 AQR**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 24.00** |
| **Upana** | - | **mita 5.45** |
| **Kimo** | - | **mita 5.20** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217156002

# Ukata ulivyo kikwazo cha matumizi nishati mbadala

**Na Grace Mwakalinga, aliyekuwa CHUNYA**

CHUNYA inatajwa kuwa miongoni mwa maeneo hatari zaidi kwa uharibifu wa mazingira nchini kutokana na uchomaji mkaa.

Mwaka 2017, yaani miaka mitano iliyopita, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilitaja Chunya kuongoza halmashauri za Mkoa wa Mbeya kwa uchomaji wa mkaa, ofisi hiyo ikitoa angalizo la athari za kimazingira dhidi ya ukataji miti.

NBS iliweka takwimu za kitafiti kwamba kuna wastani wa hekta nane za misitu kuharibiwa kila mwaka katika halmashauri hiyo kutokana na ukataji miti na uchomaji mkaa.

Ni tahadhari inayomulikwa na uongozi wa eneo hilo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya ikibainisha kuwa wilaya hiyo sasa imepoteza takriban hekta 800 za misitu kutokana na shughuli hizo.

Licha ya kuwapo angalizo hilo, wakazi wa wilaya hiyo wanakiri kutambua hatari inayowakabili kutokana na uharibifu huo, lakini matumizi ya nishati mbadala kwao ni mtihani mgumu kutokana na uwezo wao mdogo kiuchumi, wengi wakishindwa kumudu gharama za kununua gesi au kutumia majiko ya umeme katika kupika chakula.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Upatikanaji wa Nishati nchini ya mwaka 2017, Mkoa wa Mbeya unatumia kuni kwa asilimia 68 na mkaa asilimia 7.4 kwa ajili ya kupikia, kiwango ambacho ni cha juu kulinganisha na matumizi ya nishati ya umeme.

Katika kuhakikisha wananchi wanahimizwa matumizi ya nishati mbadala ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, jitihada mbalimbali za kunusuru wilaya hiyo zimekuwa zikifanyika.

Jitihada hizo ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya kinyesi cha wanyama, nishati inayotajwa kuwa rafiki wa mazingira. Ni mkakati uliopata uungwaji mkono kutoka kwa wananchi wakimo wa Kijiji cha Itumba, Kata ya Chalangwa wilayani Chunya ambao wameranzisha mradi wa nishati inayotumia kinyesi, wakitumia kwa kupikia na hata kupata mwanga.

Mradi huo unaotekelezwa chini ya ufadhili wa Shirika la Catholic Reif Services, ulianzishwa wilayani humo mwaka 2017 kwa lengo la kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kusaidia wananchi kuachana na uchomaji misitu kwa ajili ya kupata mkaa.

David Mwakatundu, mkazi wa Kijiji cha Itumba, anasema walianzisha mradi huo baada ya kuhamasishwa na wadau wa mazingira kutumia nishati itokanayo na kinyesi cha wanyama katika kupikia na kupata mwanga, wakianza na kikundi cha watu 80.



Sehemu ya shughuli za kibinadamu zinazoripotiwa kuathiri mazingira katika Kijiji cha Itumba wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

Anasema mradi huo pia unalenga kusaidia kutengeneza mbolea ya samadi kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa wakazi wanaoishi jirani na mradi kwa kuwa walielezwa kuwa mbolea za viwandani, hazina ubora kulinganisha na za asili.

Anasema baada ya kupewa elimu, walihamasika na ndipo watu 14 waliokuwa tayari kuendelea na mradi huo kati ya 80 waliouanzisha, walipoamua kuchanga jumla ya Sh. milioni 1.5, wakijenga mtambo kwa kushirikiana na wataalamu wa taasisi ya CRS ya jijini Mbeya.

Mwenyekiti wa Mradi huo, Shabani Mwangomo anasema ulilenga kuzihudumia kaya 15 zinazoishi ndani ya mita 150 kutoka mahali ulipo mtambo huo.

Mwangomo anasema: "Mwaka mmoja baadaye, mradi ulisimama licha ya wananchi kuvutiwa nao. Shida ni kwamba tumeshindwa kuuendesha baada ya kukosekana kwa mtaji, hatuna ng'ombe wa kutosha kwa ajili ya kinyesi, pia hatuna mikokoteni ya kubeba samadi kutoka majumbani hadi kwenye mtambo."

Idara ya Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Chunya inakadiria wilaya hiyo kuwa na mifugo milioni 4.2. Kati yake, ng'ombe ni 327,547, mbuzi 34,447, kondoo 14,627 na idadi iliyobaki ni ya wanyama wengine wakijumuisha kuku, nguruwe na mbwa.

Saimon Komba, mkazi wa Itumba, anasema ili kuunganisha mfumo huo, unatakiwa kuwa na fedha kuanzia Sh. 300,000, kiasi ambacho wanakijiji wengi wanashindwa kumudu.

Kwa mujibu wa Komba, jiko la kupikia la mtambo wa nishati itokanayo na kinyesi cha wanyama linauzwa Sh. 150,000, taa kwa ajili ya mwanga Sh. 40,000 na fedha kwa ajili ya kumlipa fundi anayeunganisha mfumo huo ni Sh. 250,000.

"Pamoja na vikwazo hivyo, pia kuna umbali kutoka sehemu ilipo mifugo hadi eneo la mtambo, hali inayosababisha washindwe kufikisha samadi kwenye mtambo kwa ajili ya kuzalisha nishati," anafafanua.

Komba anataja kikwazo kingine ni kukosekana kwa wataalamu wa kutengeneza mtambo pindi linapotokea tatizo la kiufundi.

Yasinta Mwanjala, mkazi mwingine wa eneo hilo, anabainisha kuwa mtambo wake ameutumia kwa mwezi mmoja tangu ulipofungwa nyumbani kwake, ukaharibika.

Yasinta anasema kuwa baada ya kubaini hali hiyo, aliwataarifu wataalamu wa kutengeneza mtambo huo lakini hadi sasa hawajafika kuona tatizo na kuufanyia matengenezo ili uendelee kufanya kazi.

Mama huyo anaeleza kuwa na ng'ombe 26 wanaomwezesha kupata ziada ya mbolea katika mtambo huo, hivyo hana kikwazo cha upatikanaji wa malighafi bali ukosefu wa wataalamu kwa ajili ya ufundi.

"Niliufurahia sana huu mradi kwa sababu ulinisaidia kuhifadhi mazingira yetu, nilitumia zaidi ya Sh. milioni tatu kwa ajili ya kujenga mtambo huu hapa nyumbani kwangu na ndani ya mwezi mmoja nilioutumia, niliona matokeo mazuri sana," anasema.

Maria Frank anayeishi umbali wa mita 200 kutoka ulipo mradi huo, anasema matamanio yake yalikuwa kujiunga na waendeshaji wa mtambo huo lakini ndoto yake imefifia kutokana na uzalishaji kwenye mtambo kusimama, akikiri matumizi ya gesi ni ghali kulinganisha na nishati hiyo itokanayo na kinyesi cha wanyama.

"Nilishawishika sana kuona wenzangu wamejiunga na kutumia nishati mbadala ya kinyesi cha wanyama.

Nilifanya jitihada za kuonana na uongozi wao ili kufahamu jinsi ya kujiunga na namna ninavyoweza kutumia nishati hiyo lakini muda mfupi baadaye nikaona shughuli za uzalishaji zimesimama," anasema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Itumba, Joyce Stanton anasema mtambo huo umesitisha uzalishaji kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa samadi.

Anasema uzalishaji kidogo wa samadi ya ng'ombe ulichangia mtambo huo kukosa malighali za kuzalisha nishati na kusababisha mtambo kushindwa kufanya kazi. Joyce anasema mbali na kukosekana kwa samadi ya kutosha, pia hawakuwa na mtaji wa kutosha kuendesha shughuli za uzalishaji nishati hiyo, akiwa na ufafanuzi kwamba ulihitaji ukarabati wa vifaa.

"Baada ya kuona wenzetu wamepata mradi huo, ofisi ya kijiji ilionana na uongozi kufahamu namna tunavyoweza na sisi kutumia nishati hiyo lakini tulikwama baada ya kuona uzalishaji umesimama," anasema Joyce na kubainisha ofisi yake haina rasilimali za kuwezesha kuendeleza mradi huo.

Ofisa huyo anasema kusimama kwa uzalishaji wa nishati hiyo itokanayo na kinyesi cha wanyama kwenye kijiji hicho, kumechangia kuendelea kwa shughuli za ukataji misitu ovyo na kuchoma mkaa, hivyo kuchangia uharibifu wa mazingira.

"Pia baadhi ya watu hufanya biashara ya kusafirisha mkaa ili kujipatia kipato na kuendesha maisha yao na kusahau kuwa wanaiweka wilaya yao kwenye hatari ya kuwa jangwa," anahadharisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Tamim Kambona anasema mipango yao ni kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwamo itokanayo na kinyesi cha wanyama kwa kuwa itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Anasema hatua hiyo inakwenda sambamba na kuhamasisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi ili kupata mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Anasema wananchi wakijiunga kwenye vikundi na kujisajili, kutasaidia kupata fedha ambazo zitachochea matumizi ya nishati mbadala ambayo wataitengeneza na kuiuza kwa wananchi.

"Tunaendelea na opereshni mbalimbali za kuzuia na kuwakamata wananchi wanaohusika na uharibifu wa mazingira hususani wanaokata miti na kuchoma mkaa.

"Wilaya hii imeathirika kwa kiasi kikubwa na shughuli hizi. Kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama na viongozi wa vitongoji, vijiji na kata tumeweka vizuizi kwa ajili ya kuwakamata wanaohusika na uchomaji na ubebaji wa mkaa," anaeleza mikakati yao.

Kambona pia anasema wamefungua milango kwa wawekezaji kwenye nishati jadidifu ili kuunga mkono juhudi za serikali za kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya matumizi ya kupikia.

Meneja wa Barazala Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Glory Kombe anasema ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira, jamii inapaswa kutumia nishati mbadala, ikiwamo itokanayo na kinyesi cha wanyama.

Anakiri asilimia kubwa ya wakazi wa Mkoa wa Mbeya wanatumia mkaa na kuni kama nishati ya kupikia, jambo linalochangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti.

"Mara kwa mara tunatoa elimu kwa wananchi juu ya athari za kimazingira zinazotokea kutokana ukataji wa miti. Pia tunahamasisha matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza wimbi hili la ukataji miti hususani kwa Wilaya ya Chunya ambayo iko hatarini zaidi.

"Matumizi ya nishati mbadala yatasaidia kupunguza ukataji wa miti kwenye misitu yetu ya asili kwa ajili ya kuchoma mkaa, ni vyema tukajikita kwenye hili ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," Glory anahitimisha.

## TANGAZO

# TUZO KWA WALIPA KODI BORA WA 2021/2022



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Chande, (Kushoto) akimkabidhi tuzo Mwakilishi wa Benki ya NMB baada ya kuibuka mshindi wa jumla katika kipengele cha Walipakodi bora kwa mwaka 2021/2022. Tuzo hiyo imetolewa hivi karibuni jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Chande (kushoto) akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya M&P Exploration Production Tanzania LTD kwa kuwa Mlipakodi mwenye uhiari wa ulipaji wa kodi Kitaifa wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi 2021/22. Tuzo hiyo imetolewa hivi karibuni jijini Dar es Salaam.



Kamishna Mkuu wa TRA, Bw. Alphayo J. Kidata (kushoto) akikabidhi tuzo kwa mwakilishi wa shule ya sekondari ya Kibaha iliyopo mkoani Pwani kwa kuibuka kinara wa mashindano ya vilabu vya kodi kwa shule za sekondari kwa mwaka 2021/22. Shule nyingine vinara ni pamoja na St. Mary's pamoja na Chang'ombe sekondari. Tuzo hizo zimetolewa hivi karibuni wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora kwa mwaka 2021/2022 jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (kushoto) akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya Bia ya Tanzania Breweries Public Limited Company (TBPLC) kwa kuwa Mlipakodi bora kati ya walipakodi wanaochangia kiasi kikubwa cha kodi. Tuzo hiyo imetolewa hivi karibuni jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Chande (kushoto) akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya uchimbaji wa madini ya GGM kwa kuwa Mlipakodi bora kati ya walipakodi wanaochangia kiasi kikubwa cha kodi nchini wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora kwa mwaka 2021/22. Tuzo hiyo imetolewa hivi karibuni jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Chande (kushoto) akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya Simu ya Vodacom Tanzania kwa kuwa Mlipakodi mwenye uhiari wa ulipaji wa kodi Kitaifa wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi 2021/22. Tuzo hiyo imetolewa hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kombe la Dunia Qatar tulitumie kama darasa

**FAINALI** za Kombe la Dunia zinatarajiwa kufanyika kuanzia kesho ambapo mechi ya ufunguzi itawakutanisha wenyeji, Qatar dhidi ya Ecuador.

Tayari timu zote zinazotarajiwa kushiriki fainali hizo, zimeshafika Qatar kwa ajili ya kuchuana kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Licha ya Tanzania kutopata nafasi ya kushiriki fainali hizo tangu zilipoanzishwa, lakini zinaweza kutumia mashindano ya mwaka huu kama darasa kwa ajili ya kujiimarisha katika idara zake mbalimbali kuelekea michuano ijayo. Ili mechi zichezwe katika ubora wake, ni lazima kuwe na kikosi imara, maana yake klabu au taifa liwe na wachezaji wenye kiwango cha juu katika kuhakikisha wanapambana na kusaka matokeo chanya katika kila mechi.

Hii husaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa na timu au klabu husika, lakini pia huwafanya wachezaji waliopata nafasi ya kushiriki kucheza kwa juhudi kwa sababu wanahitaji kutangaza vipaji vyao na kwa wale wanaofanikiwa, basi hupandisha thamani yao kuelekea dirisha la usajili linalofuata.

Tumeshuhudia wachezaji mbalimbali kila baada ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Dunia, hupata mikataba minono lakini wale waliokuwa wakijiamini husubiri kumalizika kwa fainali hizi na kukaa upya mezani na mabosi wao kujadiliana kuhusu maslahi, na hatimaye kila upande hufanya uamuzi kwa usahihi.

Ina maana kupitia mashindano haya, tunaamini wachezaji wa Tanzania watatumia kama shule kwa lengo la kujiimarisha na pale watakaporejea uwanjani kuonyesha kile walichojifunza kupitia mataifa hayo yanayoshiriki fainali hizi za dunia. Kucheza kwa kujituma ndio msingi pekee na ndio kitakachotoa hatima ya mchezaji husika licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na makocha.

Ukiondoa wachezaji, fainali hizi za dunia zinatakiwa pia kuwarudisha darasani makocha wetu, wawe raia wa Tanzania au wageni kujifunza mbinu na mikakati ya ushindi na baadaye kuhamishia makali hayo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nipashe inaamini kocha ambaye atatumia muda wake kuangalia mazoezi kwa kufuatilia vipindi na mahojiano mbalimbali ambayo makocha wenzao wamefanya kabla na baada ya kufika Qatar, hapana shaka timu anayoifundisha inaweza kubadilika na kuwa hatari wakati huu ambapo mzunguko wa kwanza unakabiria kuelekea ukingoni.

Makocha wanatakiwa wajiamini wanaweza na wasione uvivu au aibu kuuliza kwa wakufunzi hao kupitia yale watakayoyaona katika fainali hizi, kwa sababu mwisho wa siku utahitaji kutumia mbinu na mikakati hiyo kuisaidia timu yako ifanye vizuri kwenye michuano inayoshiriki.

Ni jambo la kujivunia katika fainali za mwaka huu, timu tano za Afrika ambazo zimefuzu kushiriki mashindano hayo zinaongozwa na makocha kutoka mataifa husika, hii imedhihirisha si lazima kuamini makocha 'wazungu' ndio wenye uwezo wa kuzivusha timu kwenda katika mashindano makubwa.

Kama mwaka huu imewezekana kwa makocha wenye damu za Kiafrika kupata mafanikio hayo, basi inawezekana pia kwa kocha Mtanzania kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kama ilivyowezekana kwa Simba Queens kubeba taji la Ligi Kuu ya Wanawake Nchini kwa misimu minne mfululizo ikiongozwa na makocha wa hapa nchini.


Watu wengine wanaotakiwa kutumia michuano hii kama shule ni waamuzi, Tanzania imekuwa na kilio cha muda mrefu cha waamuzi wake kuboronga katika mechi mbalimbali hasa za Ligi Kuu Bara, naamini kupitia fainali hizi, waamuzi wetu watajiimarisha na wao watakaporejea dimbani kuonyesha ubora wao. Endapo waamuzi wetu watafanikiwa kupunguza au kumaliza makosa yao, tunaamini siku si nyingi nao watakuwa miongoni mwa maofisa watakaochezesha michuano hiyo ya juu duniani.

Maofisa wa mechi, huu pia ni wakati muhimu kwa wao kujifunza utaratibu wa mashindano, darasa sahihi kwa hili lingewezekana kama nchi ingepeleka mdau kwenye fainali hizo hata kwa njia ya kujitolea.

Ukiondoa sheria mbalimbali ambazo zinaonekana kuwa ngumu huko Qatar, lakini ni wakati mwingine muhimu kwa mashabiki wa soka kujifunza namna ya kushabikia kistaarabu, wenyeji wameahidi ulinzi ulioandaliwa haujawahi kutokea katika fainali zilizopita huku wakiwakumbusha mashabiki hao kuishi kwa utulivu muda wote watakaokuwa nchini humo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Safi TFF kuzuia 'vibabu' kucheza Ligi za Wilaya

**KATIKA** Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) uliofanyika jijini, Mwanza Jumatatu iliyopita, pamoja na mambo mengine, Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia alielekeza kuanzia sasa Ligi za Wilaya zichezwe na wachezaji vijana ambao wana umri chini ya miaka 20.

Karia akasema vijana wengi kwa sasa nchini wanashindwa kuonyesha vipaji vyao kwa sababu wachezaji wanaostaafu kucheza ligi za madaraja ya juu wamekuwa wakishuka chini na kucheza ligi hiyo na nyingine za madaraja ya chini, hivyo kuwazibia chipukizi hao kuonyesha vipaji vyao.

"Tunaelekeza mikoa kuwa Ligi za Wilaya zichezwe na vijana wasiozidi umri wa miaka 20, tunafanya hivyo makusudi kwa sababu nchi yetu imekuwa kubwa, hatuna rasilimali ya kucheza ligi za vijana, sasa utakuta vijana wanakwama kwa sababu kuna wanaostaafu huko juu, halafu wanakuja huku wanacheza tena ligi za madaraja ya chini," alisema Rais huyo.

Ni kauli ya kuungwa mkono, ingawa inaonekana kama ilichelewa sana.

Tanzania ina vituo tu vya kulelea vijana wenye vipaji, lakini haina shule maalum ambazo kwa wenzetu wanaziita 'academy' ambazo ndizo hupatikana wachezaji wengi chipukizi ambao baadaye wanakuwa si tegemeo kwenye klabu mbalimbali , lakini pia kwa taifa.

Nchi inaweza kuchezesha Ligi Kuu ya timu za vijana ambayo inazishirikisha timu za 16 za Ligi Kuu, lakini bado haiwezi kuwa ndiyo msingi mkuu wa kupata au kuvumbua vipaji kwani bado ni timu chache sana kutokana na mazingira pamoja na jiografia ya taifa hili.

Tanzania ni kubwa mno na inatakiwa kupata vipaji kutoka kila pembe ya nchi kama ilivyokuwa zamani.

Kusema kweli kitendo cha Ligi za Wilaya jinsi zilivyokuwa zikichezeshwa zilikuwa zinaminya wachezaji wengi chipukizi kuonekana.

Vipaji vinafichwa, havionekani, vijana wanakata tamaa, hawawezi kwenda sehemu nyingine yoyote kuvionyesha, matokeo yake vinafia huko kwa kuamua kufanya kazi zingine.

Tumeona baadhi ya wachezaji wakiwa wamecheza klabu kubwa tu za Ligi Kuu hapa nchini miaka ya mwanzoni wa 2000, lakini hadi leo hii wanacheza Ligi ya Wilaya na kuwaweka benchi vijana ambao nao wanataka 'kutoka'.

Kwa hali ya kawaida klabu haiwezi kumwacha mchezaji mkongwe ambaye ana uzoefu na kumtumia kijana kwa sababu tu ana kipaji, hii imesababisha nchi kubaki na wachezaji wale wale miaka nenda rudi, na inakosa wachezaji wapya vijana pamoja na vipaji vipya vya soka.

Ndiyo maana tunaona hata kwenye Ligi Kuu wachezaji mara nyingi ni hao hao tu, viwango ni vile vile na wasiobadilika tena. Mfano unaweza kuona baadhi ya wachezaji wa Biashara United, msimu ujao utawakuta wapo Mbeya City, unaofuata Polisi Tanzania, halafu Coastal Union, yaani ligi inakuwa na idadi ndogo tu ya wachezaji wazawa wapya wanaoingia na kuleta ladha mpya. Badala yake wachezaji wengi wapya ni wageni tu kutoka nje ya nchi.

Hii si afya sana kwa soka la Tanzania. Tunahitaji kila mwaka kuwa na wachezaji wapya vijana wanaingia kwenye Ligi Kuu. Wataingiaje? Ni kuonekana kwenye Ligi za Wilaya ambapo klabu za Ligi Kuu zitawaona, badala ya kukutana na wakongwe ambao wameshastaafu.

Nimkumbushe Karia tu, mbali na waliostafu Ligi Kuu , lakini pia Ligi za Wilaya zina wachezaji kibao wa kigeni, hivyo kwa kuzuia hilo, wamezuia na wageni pia.

Niongeze tu kumwambia Karia akazie kuelekeza hata hao vijana chini ya miaka 20 pia, wawe makini na wale watakaodanganya umri, lakini pia kukazia lazima wawe Watanzania, kwani wanaweza kumiminika vijana chini ya miaka 20, lakini kutoka nchi jirani hasa mikoa ya pembezoni mwa nchi kwa sababu wenzetu ni wazuri kwa kuchangamkia fursa.

Hili likifanywa kwa umakini miaka michache tu baadaye tutaanza kuona matunda yake.

## Serikali yakiri udhaifu itifaki matukio

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

IDARA ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu imesema kuna changamoto kubwa kwenye eneo la itifaki ya viongozi wakati wa sherehe na matukio mbalimbali ya kitaifa katika kuwatambua, kujua wajibu wao na masuala ya ustaarabu.

Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Batholomeo Jungu, alisema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku mbili kuhusu itifaki ya viongozi wa kitaifa yanayofanyika mjini hapa.

Mafunzo hayo yanawashirikisha wakurugenzi wa utawala na usimamizi wa rasilimali watu kutoka wizara, idara na taasisi za serikali na makatibu tawala wasaidizi wanaoshughulikia utawala na rasilimali watu kutoka mikoa yote nchini.

"Kuna changamoto kubwa kwenye eneo la itifaki ya viongozi katika kutambua viongozi wenyewe kujua wajibu wao masuala mazima ya ustaarabu mfano ukiwa kiongozi unavaaje, unakulaje kwenye tukio la viongozi wa kitaifa," alisema.

Jungu alisema kutokana na changamoto hiyo, Idara ya Maadhimisho na Sherehe za Taifa, imeandaa mafunzo hayo ili wahusika wafahamu itifaki ya viongozi kwenye matukio ya kitaifa.

Kuhusu washereheshaji binafsi kuendesha shughuli za kitaifa, alisema kimsingi serikali inapaswa kuwa na washereheshaji wake wanaojua itifaki za viongozi lakini kumekuwa na changamoto katika kuwapata.

Hata hivyo, alisema mchakato wa mafunzo umeanza kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa ili kuwatengeneza washereheshaji wazuri.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi, alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa sababu kumekuwa na upungufu mkubwa kwenye eneo la itifaki.

"Changamoto iliyopo watendaji wetu wanapenda kufanya kazi kwa mazoea wakati serikali tunafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Mafunzo haya yatawafanya wabadilike na kuanza kufanya kazi kwa kufuata taratibu zinazotakiwa," alisema.

Daudi alisema baada ya mafunzo haya, wakurugenzi wa utawala na usimamizi wa rasilimali watu kutoka wizara, idara na taasisi za serikali na makatibu tawala wasaidizi utawala na rasilimali watu wataanza kupimwa kama wanafanya kazi kwa utofauti au kwa mazoea.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema ni imani ya serikali kuwa baada ya mafunzo hayo watapata maarifa, kuongeza umakini na weledi katika kutekeleza majukumu yao.

"Katika suala la uwekaji wa bendera na matumizi ya alama za taifa kama vile wimbo wa taifa kwa uzoefu wangu nimegundua kuna ubabaishaji mwingi sana hivyo naamini mafunzo haya yatawapa majibu sahihi," alisema.

# Mgogoro mwekezaji, wananchi mbioni kutatuliwa

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya takriban miaka saba ya mgogoro wa barabara kati ya wananchi na mwekezaji kampuni ya ASM (T) Ltd katika mtaa wa Mikenge kata ya Kimbiji wilayani Kigamboni, hatimaye halmashauri ya manispaa hiyo imesema ipo mbioni kuumaliza mgogoro huo.

Mgogoro huo uliibuka baada ya ASM (T) Ltd kufunga barabara inayopita kwenye viwanja vyake kwenda maeneo mengine ya wawekezaji na pwani ya bahari, hivyo kusababisha mvutano wa muda mrefu.

Mkurugenzi wa manispaa ya Kigamboni, Erasto Kiwale, alisema juzi kuwa baada ya maagizo kutoka ngazi za juu na vikao mbalimbali vya kumaliza mgogoro huo, tayari taratibu za kiofisi zinaendelea ili kumlipa fidia mwekezaji huyo na kuvunja ukuta aliojenga kupisha barabara hiyo kutumika.

Alisema kwa sasa taratibu za kiofisi zinaendelea kwa kuwa suala la ulipaji wa fidia ni mchakato unaohusisha wataalam mbalimbali.

"Niwaombe tu wananchi na wawekezaji wa maeneo yale kuwa wavumilivu wakati suala hili likiendelea kufanyiwa kazi ndani ya ofisi. Tunafahamu ni mgogoro wa muda mrefu na sasa tumefikia suala la ulipaji fidia. Huu ni mchakato ambao kuna wataalamu mbalimbali wanahusishwa kabla ya ulipaji wenyewe na kulichukua lile eneo," alisema.

Pia alisema serikali ipo kwa ajili ya wananchi hivyo kero na shida za wananchi zinapewa uzito mkubwa.

"Lakini pia serikali inawahitaji wawekezaji. Tunachofanya ni kuweka mazingira mazuri ya Uwekezaji ili anayewekeza apate kile alichokikusudia na Serikali pia ipate inachostahili huku wananchi nao wakiendelea na shughuli zao kwa amani," alisema Kiwale.

Mkurugenzi huyo alisema manispaa inataka kuona wawekezaji wengine katika maeneo hayo ya fukwe wanapata uwezo wa kufika kwenye maeneo yao na kuendelea na biashara zao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mikenge, Lameck Mayala, alisema wanaiomba serikali kumaliza mapema mgogoro huo ili kutoa fursa kwa wananchi kuendelea na shuguli zao kupitia barabara hiyo iliyofungwa.

Alisema mgogoro huo ni wa muda mrefu na umesababisha shughuli nyingi za kiuchumi kusimama.

"Hii barabara ndiyo iliyokuwa inatumiwa na wananchi kufika baharini kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa sababu wakazi wengi wa huku wengi ni wavuvi na hii ndiyo barabara iliyokuwa inawafikisha baharini, ukiondoa wananchi, ukipita viwanja vya mwekezaji ASM, mbele kuna wawekezaji wengine wamejenga hoteli na vijana wetu wengi walipata ajira huko.

Kwa sasa hoteli zimefungwa na watoto wetu wengi wamepoteza ajira. Tunaomba serikali kwa sababu tayari wamekiri kuufanyia kazi, basi mchakato uharakishwe jambo hili liishe," alisema Mayala.

Mmoja wa wawekezaji wa hoteli katika maeneo hayo, Vidate Msoka, aliiomba manispaa kuharakisha kumaliza mgogoro huo ili barabara hiyo ifunguliwe na waendelee na biashara zao.

"Kwa sasa hakuna kinachoendelea, biashara zimesimama tulilazimika kuwaondoa watu kazini kwa sababu hakuna wageni wanaokuja kutokana na kufungwa kwa barabara hii. Tunaomba mchakato huu uharakishwe kwa sababu ni mgogoro wa muda mrefu," alisema.

Mwekezaji mwingine, Arif Sheikh, alisema wanashukuru kwa hatua ambayo Manispaa ya Kigamboni imechukua lakini anaomba kuharakishwa mchakato wa kumlipa fidia mwekezaji huyo aliyefunga barabara.

Mgogoro huo wa barabara uliibuka baada ya mwekezaji ASM anayemiliki viwanja viwili pacha kwenye eneo hilo kupinga kuwapo kwa barabara iliyopita katikati ya viwanja hivyo na kuvitenganisha.



Wamachinga wakifanya biashara katikati ya njia ya mabasi ya mwendokasi inayoendelea kujengwa katika Barabara ya Kilwa, eneo la Mbagala Rangi Tatu, Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Soko pilipili kichaa lawaliza wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MASOKO ya pilipili kichaa yaliyoko Ulaya yamevurugika kutokana na vita kati ya Russia na Ukraine na kusababisha vilio na hasara kwa wakulima nchini.

"Tumebaki gizani na pilipili zetu tulizovuna baada ya wanunuzi tuliokuwa na makubaliano ya kununua zao hili na kusafirisha kwenda kwenye masoko ya Ulaya kutokuonekana," alisema Emmanuel Laizer, mkulima wa pilipili kutoka Arusha alipozungumza na Nipashe jana.

Mmoja wa wanunuzi wa zao hilo ni kampuni ya Vitesse ya jijini Dar es Salaam ambayo imekiri kushindwa kutimiza makubaliano yake na wakulima hao kwa kuwa soko la Ulaya limevurugika kutokana na vita tajwa. "Kampuni inaomba radhi kwa usumbufu na hasara waliyopata wakulima hasa kwa wale wenye mikataba na sisi," taarifa ya kampuni hiyo inabainisha.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, masoko ya pilipili kichaa kutoka mwezi Aprili mwaka huu yamekuwa na vikwazo kutokana na sababu mbalimbali hasa vita vya Russia na Ukraine.

Kampuni ya Vitesse katika taarifa yake hiyo ilibainisha kuwa ilikuwa inategemea zaidi masoko ya Ulaya, ikifafanua: "Hali hii imesababisha kudorora kwa soko letu la ndani na kuleta hasara kubwa kwa kampuni na wakulima wa pilipili kichaa." Taasisi Asasi ya kilele ya sekta binafsi inayojihususha na kuendeleza tasnia ya horticulture -- maua, mboga za majani, matunda, mimea itokanayo na mizizi na viungo nchini (TAHA), imekiri kuwapo shida ya kukosekana kwa masoko ya pilipili kichaa na inafanya jitihada za dhati kutafuta masoko ya kikanda ili kuwanusuru wakulima.

"Kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa zao la pilipili kichaa (African Birds-Eye Chili) kutokana na fursa kubwa za masoko hasa ya nje.

"Hata hivyo, mwenendo wa bei ya zao hilo unaonesha bei imeshuka kuanzia mwezi Juni mwaka huu, hivyo kusababisha wakulima wengi kukosa soko," alisema Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi. Dk. Mkindi alisema TAHA inafanya jitihada za kuwezesha kununuliwa kwa mzigo wote wa pilipili kichaa uliopo kupitia wanunuzi watakaopatikana na kuwashauri wakulima kulima mazao mbadala yatakayothibitika kuwa na uhitaji kwenye masoko.

# NBC yateuliwa kusimamia uwekezaji mamlaka maji

Na Joseph Mwendapole

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Uwekezaji (UNCDF) limetangaza rasmi uteuzi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kuwa mtaalam mshauri atakayekamilisha hatua za msingi kuwezesha kuuzwa kwa hati fungani ya Mamlaka ya Maji Tanga (Tanga UWASA) ambayo itakuwa ya kwanza kuwahi kutolewa na taasisi ya serikali nchini.

Uteuzi huo umeambatana na utiaji saini wa makubaliano ya kimkakati baina ya UNCDF na NBC ambayo itaongoza timu ya wataalamu washauri inayojumuisha taasisi tano zinazotoa huduma za ushauri wa kifedha na uwekezaji na kusajiliwa na Mamlaka ya Masoko ya Hisa na Mitaji (CMSA).

Hatua hiyo ya uteuzi ni kwa mujibu wa matakwa na miongozo ya CMSA na timu hiyo inatarajiwa kuhakikisha hati fungani ya mamlaka hiyo ya majisafu na usafi wa mazingira inaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ifikapo robo ya kwanza ya mwaka 2023.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utiaji Saini, Mkurugenzi wa Tanga UWASA, Geoffrey Hill, alisema siku hiyo muhimu imefikiwa kutokana na ushirikiano wao na UNCDF na kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya serikali ya kutafuta vyanzo mbadala vya fedha ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Tunatarajia kufanya kazi kwa ukaribu na NBC ili kuharakisha hatua zilizobaki kuwezesha upatikanaji wa fedha zitakazotumika kuboresha na kuongeza uwezo wetu wa kusambaza maji kwa wananchi na maeneo yasiyo na huduma hiyo" alisema.

Mkuu wa UNCDF Tanzania, Peter Malika, alisema: "Tunajivunia kuwateua NBC ambayo ni taasisi ya kitanzania kukamilisha suala hili la kihistoria. Hii ni njia mojawapo ya kuimarisha na kujenga uwezo wa ndani kuibua na kutumia vyanzo bunifu vya fedha kugharamia maendeleo.

"UNCDF kama mdau wa maendeleo ina nafasi muhimu ya kusaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha husuani kwenye nchi zinazoendelea ambazo masoko ya fedha ni machanga," alisema.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa NBC, James Meitaroni, alisema: "Tukiwa benki ya kizalendo, tunajivunia kuwa taasisi ya kifedha ya kwanza nchini kushiriki kama kiongozi wa mchakato na mtaalam mshauri, katika kuhakikisha ukamilifu na uuzwaji wa hati fungani hii ambayo itakuwa ni ya kwanza kutokea Tanzania. Tumeshuhudia historia ikiandikwa kwa mara ya kwanza nchini, mamlaka ya umma imefungua milango mipya ya kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo," alisema.

Aidha, alisema fedha zitakazopatikana kutoka kwenye mauzo ya hati fungani zitaenda moja kwa moja kurekebisha miundombinu ya maji ya mji wa Tanga na hivyo kuongeza tija ya upatikanaji na usambazaji maji jijini Tanga.

"Tunajivunia kuwa Benki washauri na kutumia uzoefu wetu katika kuleta suluhu ya changamoto zinazokabili jamii. Kupitia hati fungani hizi tunaenda kupata suluhu kubwa ya tatizo la upungufu wa mji mkoani Tanga na vijiji vya jirani.

" Tunaishukuru sana serikali na wadau wengine kama UNCDF kwa kuendelea kuweka mazingira bora yanayofanya taasisi za kifedha kama sisi NBC kushiriki katika shughuli za kutatua changamoto za jamii inayotuzunguka," alisema.



Kamishna wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Said Athuman (kushoto), akikabidhi cheti cha mlipakodi bora kwa mwaka 2022 kwa wajasiriamali wa kati wa Wilaya ya Ilala, kwa Mkurugenzi wa kampuni ya Chanika Poultry Farm, Martin Balige, katika hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora 2022, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwili wa mtoto wakutwa katika shimo majitaka

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MWILI wa mtoto Mwasiti Adamu (7), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Majengo, umekutwa umetumbukizwa kwenye karo la majitaka mtaa wa Lumelezi, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Akizungumzia tukio hilo, baba mzazi wa mtoto huyo, Adam Kwandikwa, alisema Mwasiti alikuwa anacheza na watoto wenzake eneo ambalo anafanya biashara majira ya saa moja jioni Novemba 14, mwaka huu, na alipotea kusikojulikana.

Rashid alisema Jumatatu na Jumanne, familia katika harakati za kumtafuta, walifunua mfuniko wa karo na walipokoroga waliona ndala aliyokuwa amevaa na baadaye mwili wake huku akiwa tayari amekufa.

Baba mdogo wa marehemu, Ramadhani Rashid, alisema mtoto huyo alikuwa akiishi na mama wa kambo, Scholastica na dungu zake ambao wamechangia baba.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi linawashikilia mama wa kambo na Mwajuma Sylvester ambaye aliwahi kuwa mke wa baba wa marehemu kabla ya kuachana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janet Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

# Mwenyekiti UWT Mkoa wa Pwani ataganza vipaumbele

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Pwani, Zaynab Vulu, amesema kipaumbele chake cha kwanza ni kushirikiana na viongozi wengine kufuatilia maadili ya watoto shuleni.

Vulu aliyasema hayo juzi mjini hapa muda mfupi baada ya kutangazwa kuwa mshindi wa nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika Picha ya Ndege.

Alisema moja ya mambo ambayo atayapa kipaumbele ni kupita shuleni kuangalia taratibu zao na ni kwa nini watoto wengi wanaharibiwa kimaadili na watu wazima na wengine wenyewe kwa wenyewe. "Watoto wetu wanaharibiwa na watu wazima. Nitapita kuangalia kwa nini haya yanatokea nini kifanyike kukabiliana na hili na kufanya matukio haya yasiendekee kutokea," alisema. Aidha, Vulu alisema anatarajia kufuatilia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwenye halmashauri ambayo wanawake ni miongoni mwa wanufaika kwa kufuatilia vikundi vinavyokopa na hali ya urejeshaji.

"Ili kufanikisha malengo yote hayo, nategemea kupata ushirikiano kutoka kwa wanawake walionichagua pamoja na viongozi kutoka sehemu mbalimbali. Mshikamano utatuwezesha kufanikisha haya," alisema.

Awali, akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Abdullah Hassan, alisema wagombea nafasi ya mwenyekiti walikuwa wanne na kura zilizopigwa zilikuwa 358.

Alisema Vulu alipata kura 320 akifuatiwa na Joan Tandau kura 38 Safihuna Singo na Rehema Ngatanda kura moja kila mmoja.

Hassan alimtangaza Mariam Ibrahim kuwa mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa baada ya kupata kura 188 akifuatiwa na Nancy Mtalemwa (165) na Judith Mluge kura tatu kati ya kura 357 zilizopigwa huku moja ikiharibika.

# Minde mwenyekiti mpya UWT K'njaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKILI mkongwe na mtetezi wa haki za binadamu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Elizabeth Minde, 'ameula' katika nafasi ya Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kumbwaga kwa tofauti ya kura 30, mwenyekiti wa zamani, Zuhura Chikira.

Minde alishinda kiti hicho, baada ya kupata kura 232 dhidi ya mpinzani wake aliyeambulia kura 202. Wagombea wengine walikuwa Cecilia Msinga aliyepata kura moja na Hellen Munisi ambaye hakupata kura.

Uchaguzi huo uliokuwa na mshikemsike kutokana na aina ya wanasiasa waliokuwa wanapambana ili kushika wadhifa huo, unatajwa kutaka kuponya majeraha yanayoitesa jumuiya hiyo kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Matokeo ya uchaguzi huo, yalitangazwa jana mjini hapa na Msimamizi wa Uchaguzi, Edward Mpogolo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Same. Minde pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya kichama ya Moshi Mjini.

Aidha, Mpogolo alimtangaza Mkuu wa Wilaya Mstaafu wa Morogoro, Regina Chonjo, kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa, baada ya kushinda kwa kura 296, dhidi ya mpinzani wake, Joyce Ndosi aliyepata kura 78 na Elizabeth Msaki aliyepata kura 62.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Minde alisema uchaguzi umekwisha na hakuna adui wa kudumu kwenye siasa, hivyo yeye na jumuiya hiyo sasa wanaungana kufanya kazi za chama pamoja na kuwafikia kinamama walioko vijijini ili nao kutambulika na kusimama kutetea chama hicho.

"Wakati wa Bwana ukifika hakuna wa kukuzuia, hakika leo (jana) ndiyo siku aliyoifanya Bwana. Sasa niko tayari kukitumikia chama na kinamama sasa tuvunje makundi ya Chikira na Minde na tutambue tuna kazi kubwa ya kukipigania chama ili kufikia malengo katika chaguzi za serikali zilizoko mbele," alisisitiza.

Chikira, mbali ya kumpongeza Minde, alisema kwenye ushindani lazima mmoja ashinde na kwamba kukosa nafasi hiyo hakutamfanya ashindwe kuendelea kushirikiana na kinamama katika kuhakikisha wanakijenga chama.

Baada ya uchaguzi huo, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akizungumza na wajumbe wa mkutano huo wa uchaguzi, alisema demokrasia imeamua nani awe kiongozi wa UWT mkoa wa Kilimanjaro na kwamba sasa ni muda wa kuvunja makundi na kuungana kufanya kazi kukipigania chama.

# Mhitimu darasa la saba akutwa mjamzito, adai mhusika shemeji

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MHITIMU wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Lemosho iliyoko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, ambaye anasubiri kutangazwa kwa matokeo ya mitihani ya taifa, amepata ujauzito baada ya kudanganywa na shemeji yake kwamba akifanya naye mapenzi atapona ugonjwa wa kutokwa damu unaomsumbua.

Msichana huyo (jina limehifadhiwa), baada ya kuhojiwa na kufanyiwa vipimo vya kitabibu katika Hospitali ya Wilaya hiyo, amegundulika kuwa na ujauzito wa miezi sita.

Jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Matadi, Asanterabi Ng'onda, akizungumzia tukio hilo, alikiri ni kweli msichana huyo amepata ujauzito na mtuhumiwa aliyetajwa na mtoto huyo ni shemeji yake.

"Ni kweli ofisi yangu imepokea taarifa hiyo kutoka kwa ndugu wa msichana, kwamba binti yao amepewa ujauzito na shemeji yake. Jambo hilo kwangu mimi kama mzazi limenisikitisha sana.

"Mtoto anasubiri matokeo ili ajiunge na kidato cha kwanza, lakini mtu anadiriki kufanya mapenzi na mtoto mdogo. Hii haipendezi kwenye jamii, tumeanza kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia ili kudhibiti wimbi la matukio haya," alisema.

Inaelezwa kuwa msichana huyo alipata ujauzito huo katikati ya mwaka huu, wakati akipewa dawa ya kuzuia kutokwa na damu puani na sehemu za siri.

Akizungumza na timu ya wanaharakati wa haki za binadamu wanaofuatilia tukio hilo, ndugu wa msichana huyo alisema: "Shemeji alimwambia ili kizazi kisioze kutokana na kutoka damu sehemu za siri ni lazima afanye naye mapenzi ili dawa ifanye kazi. Sasa sisi hatujui kama ni mganga wa kienyeji alimweleza hivyo au ni shemeji tu tamaa zake hatujui."

Alisema kabla ya msichana huyo kupata ujauzito, shemeji yao aitwaye Abed Salim, ndiye aliyekuwa akishughulikia tatizo la mtoto huyo ili apone maradhi yanayomsumbua na kurejea shuleni kuendelea na masomo yake.

"Tulimpa kazi ya kumshughulikia msichana huyo kwa sababu tatizo lake lilikuwa la mara kwa mara. Aliondoka naye Lemosho na kwenda kwa mganga wa kienyeji huko mkoani Tanga ili kutafuta tiba na alifanikiwa hadi huyo mtoto akapona.

"Lakini cha kushangaza, baada ya muda tumemkuta mdogo wetu ana ujauzito, wakati bado anasubiri matokeo ya darasa la saba. Ikabidi tumhoji ni nani amempatia ujauzito huo, alikuwa hataki kusema, tukambana na akamtaja shemeji yake kwamba ndiyo aliyempa ujauzito na akasema aliupata wakati shemeji akimpa dawa za kuzuia damu kutoka puani na sehemu za siri," alisema.

Mratibu wa Kukuza Usawa kwa Elimu ya Haki za Binadamu wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO linalotekeleza mradi huo katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, Consolatha Kinabo, alisema licha ya kazi kubwa inayofanywa ya kubomoa mawazo mgando ya jamii na kupaza sauti kukemea vitendo hivyo, bado nguvu zaidi zinahitajika kupambana na ongezeko la matukio ya ulawiti, ubakaji na unajisi katika Wilaya ya Siha, kwa kuwa ni eneo tishio la ukatili.

Kinabo alisema tayari wamependekeza kwa serikali za vijiji na kata, kila wakati kutolewe elimu ya sheria na madhara ya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto pamoja na kurejewa taratibu za kimila zinazokinzana na misingi ya haki za binadamu.



Mwongoza ndege wa kiwanja cha ndege cha Arusha, Mgaza Kigolo (wa pili kushoto), akifafanua jambo kuhusu wanavyoongoza ndege zinazotua na kupaa kwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wa nne kulia), alipotembelea kiwanja hicho, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Achomwa kisu tumboni akitoka kuangalia mpira

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Lolovoni katika Kata ya Sokoni 1, Wilaya ya Arusha, Haji Abdallah, amevamiwa na kujeruhiwa vibaya kwa visu tumboni na kundi la wahalifu la watu wanaojiita 'tatu mzuka'.

Abdallah alikumbwa na tatizo hilo wakati akitoka kwenye mabanda ya mpira kuangalia mchezo wa ligi kuu ya NBC, kati ya timu ya Simba na Namungo, uliofanyika Jumatano Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

Kundi hilo lilimvamia mwananchi huyo na kumchoma kisu tumboni hadi kuutoa utumbo nje, baada ya kuchelewa kuwapa pesa alizokuwa nazo mfukoni, simu na vitu vingine vya thamani.

Akizungumza na Nipashe jana akiwa nyumbani kwake, Haji alisema Novemba 16 mwaka huu, majira ya saa 3:00 usiku, wakati akitoka kuangalia mpira kwenye mabanda ya mpira yaliyoko karibu na makazi yake, alikutana ana kwa ana na kundi hilo na aliposimama kujua kulikoni, alisikia mmoja wa wahalifu hao akimwambia mwenzake, choma kisu shingoni.

"Nilipotoka kwenye mpira narejea nyumbani kwangu. Nilikuwa naongea na simu na nilipokaribia nyumbani niliwaona vijana zaidi ya wawili ambao walinipita wakaenda mbele na kusimama wakawa wanaongea. Baadaye nikaona wanarudi tena na mimi nikashtuka, nikakata simu. Kabla sijaweka mfukoni.

"Nilipojizuia kwa mkono, kikanikata vidole. Hapo hapo wakati nahangaika kujiokoa, mmoja akanichoma kisu tumboni, akavua viatu akaanza kukimbia na mimi nikajitahidi kukimbia kwenda nyumbani lakini nikiwa nakaribia nikawa nasikia kitu kinashuka chini kumbe ni utumbo ulikuwa umetoka nje.

"Mungu mkubwa, nikafika nyumbani na niliposimama kujikagua, kuna mzee akaniomba akasema nisishike tumbo, utumbo upo nje. Muda huo huo akaja mama mmoja, akanifunga na kanga na nikakimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru," alisema.

Akisimulia kisa hicho, kaka wa majeruhi huyo, Ramadhan Msangi, alisema siku ya tukio hilo, alikuwa na mdogo wake kwenye mabanda ya mpira wakitazama mchezo huo lakini baadae aliondoka kwenda nyumbani kwake na alipofika ghafla alipigiwa simu kuarifiwa juu ya tukio hilo.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Justine Masejo, hakupatikana kutokana na simu yake kuita bila majibu mara kadhaa.



## Aibuka kidedea uenyekiti UVCCM

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KADA wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Saimon Iranghe, ambaye ni mtoto wa Meya wa Jiji la Arusha, Maximillian Iranghe, ameibuka kidedea katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM) Mkoa wa Arusha.

Jana, Msimamizi Mkuu wa uchaguzi huo, Thomas Apson, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, alimtangaza Iranghe kuwa mshindi wa kiti hicho, baada ya kupata kura 345 kati ya kura 555 zilizopigwa.

Akitangaza matokeo hayo usiku wa kuamkia jana, Apson alisema uchaguzi huo uliofanyika kwa uhuru na haki, kada huyo na mfanyabiashara wa Jiji hilo, aliwashinda wapinzani wenzake akiwamo Ikoyo Laizer aliyepata kura 155, Nicomed Josephat aliyeambulia kura nne na Mwinyi Njuhe, aliyepata kura nane.

Kutokana na kumalizika kwa amani uchaguzi huo, Apson, aliwashukuru wajumbe kwa kufanya uchaguzi huru na wa haki, huku akimfunda Mwenyekiti huyo mpya wa UVCCM kumaliza tofauti na wapinzani wake na kuvunja makundi ili kurejea kujenga chama imara.

Baada ya uchaguzi huo kumalizika, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, aliwasihi wajumbe hao kuendelea na chaguzi nyingine ndani ya jumuiya ngazi ya mkoa.

"Nawaomba na kuwasihi wanachama wa CCM Mkoa wa Arusha, kuwa watulivu ili tumalize chaguzi zetu salama ila msisahau kwenda kutangaza yale yote mazuri yanayofanyika na yanafanywa na Mwenyekiti wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Alipopewa nafasi ya kushukuru, Saimon Iranghe, aliwaomba wanachama wa UVCCM mkoa wa Arusha, kufanya kazi kwa ushirikiano, akisisitiza uchaguzi umekwisha na wote sasa ni kitu kimoja.

# Aahidi kumpigia debe Samia 2025

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa zamani wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Mkoa wa Arusha, Yasmine Bachu, amesema hatachoka kumpigia debe Rais Samia Suluhu Hassan, ateuliwe kugombea kiti hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, hata kama atachukiwa na baadhi ya wana CCM wenzake.

Bachu aliweka wazi msimamo wake huo jana jijini hapa alipopewa nafasi ya kuwaaga wana CCM baada ya kunga'tuka katika medani ya siasa. Alikuwa akizungumza katika mkutano wa uchaguzi wa kumchagua mrithi wake.

"Mimi naondoka, lakini msisahau kalenda yetu ya kuunganisha nguvu kumchagua Rais Samia 2025 ili ashinde kwa kishindo; na hii ndio itakuwa heshima kubwa tunayoweza kumpa mwanamke mwenzetu. Ni vizuri siku zote mnapokuwa kwenye vikao vyenu mkumbushane juu ya hilo.

"Katika ushindi wa Rais Samia, pia mhakikishe kura nyingi zinatoka Mkoa wa Arusha ili kumpa heshima, kwa kazi nzuri anazofanya nchini na hapa mkoani kwetu. Kabla ya kumchagua, kazi kubwa mnayotakiwa kuifanya kwa sasa ni kutangaza kazi za Rais Samia Suluhu Hassan , anazofanya nchini ili kila mtu azifahamu na sio kuleta unafiki katika kuzisemea kazi nzuri anazofanya," alisema.

Pia Bachu aliwasihi viongozi hao wahakikishe wanabuni vyanzo vipya vya mapato na kuendeleza yale aliyoacha ili jumuiya hiyo mkoa wa Arusha, isonge mbele kiuchumi.

"Siasa bila uchumi imara haitokaa ikamilike. Ndugu zangu wana CCM, katika kila kata, wilaya na mkoa, UWT hakikisheni mnaanzisha miradi na katika hili ninaomba sana UWT iwe mstari wa mbele. Niwaombe sana viongozi pia wasiwe wanyonge katika kusimama kidete kutetea maslahi ya wanawake, kwa sababu uongozi wenye woga unakuwa haujakamilika.

"Niwasihi sana myavunje makundi na matabaka ya kampeni za uchaguzi. Tungane tuwe wamoja, kwa sababu hakuna mshindi, bali mshindi ni UWT na chama, na hapa Jumuiya imepata viongozi sio ushindi wa mtu mmoja mmoja. Tukielewa hili hatuwezi gawanyika," alisema.

Katika mkutano huo wa uchaguzi, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa wa Arusha, Flora Zelothe, amechaguliwa kuwa mwenyekiti mpya baada ya kupata ushindi wa kura 246 dhidi ya mpinzani wake, Neema Mollel aliyepata kura 155 na Agness Mbise aliyepata kura nne.




Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akimwapisha Ofisa wa Jeshi la Polisi, Issaya Mwanga, kuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji katika Kikao kilichofanyika jijini Dodoma, jana. **PICHA: WMNN**

# Mfumo maalum kuwabana madalali wa ndizi

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

SERIKALI imesema inakuja na mfumo maalum wa uratibu wa taarifa mbalimbali za bei na masoko ya ndizi ili kuwabana watu wa kati maarufu kama madalali, ambao wamekuwa wakinufaika kwa kunyonya jasho la wakulima nchini.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Kilimanjaro, James Bwanali, akieleza jana juu ya mpango huo, alisema ili kumaliza tatizo la ulanguzi wa bei ya mazao ikiwamo ndizi na bidhaa mbalimbali za chakula, serikali hivi sasa inakamilisha mfumo wa kidijitali utakaokuwa mwarobaini wa kuwaondoa madalali sokoni.

"Tunaamini kwamba hili litasaidia kurahisisha ufanyaji wa biashara. Katika mfumo huo watapata taarifa za masoko, bidhaa zao pamoja na bei. Mfumo huu ni ufumbuzi wa kuondoa tatizo la upandaji wa bei za bidhaa. Wananchi wataondokana na adha ambayo kwa sasa wanaipata," alisema.

Bwanali alivunja ukimya kuhusu madalali, baada ya Kampuni ya Kimataifa ya East Africa Foods, kufungua milango ya masoko ya zao la ndizi katika Wilaya za Rombo na Moshi, mkoani Kilimanjaro. Neema hiyo ya masoko ya uhakika ya zao la ndizi, inalenga kuwanufaisha wakulima zaidi ya 15,000 mwaka ujao, baada ya kufunguliwa kituo kipya cha kukusanyia ndizi eneo la Mamsera, Wilaya ya Rombo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya EA Foods, Elia Timotheo, akizungumzia soko hilo maarufu kama 'SokoChap' alisema uamuzi wa kufungua soko hilo unatokana wakulima wa ndizi kupata hasara kila mwaka kutokana na kukosa soko la uhakika, huku madalali wakijitajirisha nyuma ya jasho la mkulima.

"Zao la ndizi limekuwa likipata uharibifu, kwa sababu ya kukosa soko. Ndizi zinaharibika shambani, ndizi zinaharibika barabarani. Sisi tukaona hiyo ni fursa ya kuweza kuongeza kiwango cha kununua ndizi na kutumia utaalamu wa kuzihifadhi, kuzisafirisha na kuzisambaza kwa wateja ili kumaliza tatizo la ndizi kuharibika kwa kukosa soko.

"Tunao mkakati wa kufungua masoko ya nje katika nchi saba wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Huu tulioanza ni msingi kwa wakulima kuzalisha mazao mengi na bora zaidi. Soko ni kubwa na ndio maana jina letu ni EA Foods. Hiyo ni kwa sababu tunaamini kwamba lengo la kampuni ni kuweza kwenda katika nchi nyingine," alisema.

Kituo hicho cha Mamsera, kilichoko wilaya ya Rombo, kina uwezo wa kukusanya mikungu 1,000 kwa siku, tofauti na awali ambapo kilikuwa kikikusanya mikungu 500.

Kuhusu soko hilo, Mratibu wa Operesheni za Ndizi wa EA Foods katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Firmina Joseph, alisema mnyororo wa thamani wa zao hilo ambao wanaufanya kupitia kampuni hiyo, una nia ya kufuta watu wanaoitwa madalali.

"Pia mnyororo huu wa thamani tunaoufanya unalenga kufanikisha bidhaa ya ndizi inayotoka shambani, kumfikia mlaji wa mwisho, ikiwa katika thamani yake ile ile. Kama ndizi (mkungu) inauzwa Sh. 15,000 inatakiwa imfikie mlaji wa mwisho ikiwa na thamani ile ile na si inamfikia mlaji ikiwa na thamani ya Sh. 3,000 au 5,000 ni kosa.

"EA ilikataa kuwatumia madalali, ikasema haiwezi kutoka Dar es Salaam iende ikanunue ndizi Moshi au Rombo impelekee Dar es Salaam, kwa sababu mwisho wa siku atawalangua wakulima. Kimsingi, uwezo wa kituo ni kukusanya ndizi kutoka kwa wakulima kwa mwaka 2021 ulikuwa tani 5,400 lakini kufikia mwaka huu kiliongeza uwezo na kufikia tani 7,257," alisema.



## Wateja wahadharishwa wizi sokoni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UONGOZI wa soko kuu la Majengo, jijini Dodoma umewataka wateja wa soko hilo kuwatumia vijana wabeba mizigo waliosajiliwa na wenye sare maalum ili kutoangukia kwenye mikono ya wezi.

Hatua hiyo imetokana na malalamiko kutoka kwa wateja wanaotumia soko hilo kuhusu kuibuka kwa baadhi ya vijana wanaobeba mizigo wasio waaminifu.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Majengo, Godson Rugazama, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malalamiko kutoka kwa wateja ambao wamekuwa wakiibiwa vifurushi na mizigo.

Alisema kwenye soko hilo kuna vijana ambao wamevaa sare na zina namba zilizosajiliwa hivyo wateja wanapaswa kuwatumia hao na si vinginevyo.

"Wasitumie vijana ambao hawatambuliwi na uongozi wa soko, niwaombe wateja wetu wenye kuhitaji kubebewa mizigo yao, wahakikishe wanawatumia vijana waliovaa sare zenye namba hao ndiyo wamesajiliwa na uongozi wa soko wanawatambua na siyo vinginevyo," alisema.

Ili kulidhibiti tatizo hilo, Rugazama alipiga marufuku vijana ambao hawajasajiliwa kubeba vifurushi vya wateja.

Mmoja wa mfanyabiashara wa soko hilo, Pascal Maliki, alisema kuna wimbi la vijana wanaotafuta kazi za kubeba mizigo na vifurushi wako wengi baina yao wapo waaminifu na wasio kuwa na uaminifu.

Alisema kutokana na wimbi la vijana kuwa wengi, uongozi wa soko umeamua kuwasajili vijana hao ambao kazi yao kubwa ni kubeba mizigo ya wateja ili kuondokana na na malalamiko.

# Viongozi wazazi CCM wafundwa kukemea udhalilishaji wa kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), wametakiwa kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukiukwaji wa maadili ikiwamo ndoa za jinsia moja.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Katibu Mkuu wa Wazazi, Gilbert Kalima, alisema dhima na jukumu la jumuiya hiyo ni kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukiukwaji wa maadili, hivyo linapaswa kubebwa na viongozi hao.

"Tunatakiwa kuweka viongozi watakaopinga, ambao watahakikisha jumuiya yetu inakuwa kiongozi katika kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia, kupiga vita masuala ya ndoa za jinsia moja na ukiukwaji wowote wa maadili katika nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunatekeleza wajibu wetu na kanuni ya jumuiya yetu," alisema.

Pia aliwataka wajumbe kufanya uamuzi wa busara wa kutengeneza timu itakayojipanga kwa kipindi cha miaka mitano inayokuja kufanya kazi ipasavyo na kuimarisha chama.

Alisema uchaguzi huo ni wa kutengeneza safu ya kukipatia ushindi chama katika uchaguzi mbalimbali ikiwamo uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Mnatengeneza safu ya ushindi wa CCM mwaka 2025. Mkipiga kura mkumbuke kwamba mnatengeneza viongozi watakaotuongoza kwenye ushindi wa CCM mwaka 2025 na ushindi wa CCM katika chaguzi zozote zitakazofanyika,"alisema.

Alitaka kwa kipindi cha miaka mitano ijayo jumuiya hiyo iweke mikakati ya kujiimarisha kiuchumi.

"Mjielekeze katika kuweka mipango na mikakati ya kuhakikisha jumuiya yetu inaondoka hapa ilipo na kujiimarisha kiuchumi kadri inavyowezekana,"alisema.

Katibu mkuu huyo alisema kwa miaka mitano ijayo, wahakikishe chama kinakuwa imara zaidi kwa kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

"Jumuiya iunge mkono jitihada zote zinazofanywa na serikali kuleta maendeleo kwa wananchi, tumuunge mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan," alisema.

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Dk.Damas Mukasa, alihimiza wanachama kuendelea na umoja walioonyesha wakati wa uongozi wake ili kusimamia sera ya jumuiya na uchumi.

Naye msimamizi wa uchaguzi huo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema wasimamizi wa uchaguzi huo hawana wagombea bali wanatekeleza wajibu wao wa kuhakikisha uchaguzi unafanyika salama.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akimwapisha Ofisa wa Jeshi la Polisi, Issaya Mwanga, kuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto, Uokoaji na Uhamiaji katika Kikao kilichofanyika jijini Dodoma, jana. **PICHA: WMNN**

# Wananchi wapigiwa debe umeme wa REA

**Na Mwandishi Wetu,** KONDOA

SHIRIKA la Umeme Tanzania TANESCO Mkoa wa Dodoma limehamasisha wananchi wa vijiji vinavyonufaika na miradi ya umeme inayoendelea wilayani Kondoa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuchangamkia fursa hiyo ili kuunganishiwa kwa gharama nafuu.

Aidha, wametakiwa kujiepusha na vishoka pamoja na matumizi yasiyo sahihi ya umeme.

Akizungumza jana na wananchi wa vijiji vya Kikilokati, Berabera na Kwahengwa kata ya Kikilo, wilayani hapa, Ofisa Uhusiano wa Shirika hilo, Sarah Libogoma, alisema wananchi wa maeneo hayo wanapaswa kujitokeza kuomba huduma kadri serikali ilivyokusudia kwa kuwa gharama za mradi huo zimepunguzwa sana kwa wananchi.

"Kwa Sh. 27,000 unakuwa umepata huduma kwa pesa ambayo ukiuza kuku wawili unaunganisha huduma ya umeme milele kwenye nyumba yako hivyo ni vyema kuhakikisha tunatumia fursa hii vizuri kwani mradi upo ukingoni kukamilika," alisema Libogoma.

Pia aliwataka kuzingatia usalama katika matumizi ya umeme ikiwamo, kutofanya shughuli zote chini au karibu na miundombinu ya umeme kama vile transfoma na kutumia mafundi wanaotambulika wa kuweka nyaya za nyumba zao.

"Msikate miti iliyo karibu na nyaya za umeme bila kushirikiana na uongozi ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza," alisema.

Libogoma alisisitiza utunzaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwa serikali inatumia gharama nyingi katika kupeleka miradi hiyo kwenye maeneo yao ili wajikwamue kiuchumi.

Diwani wa Kikilo, Yuda Daniel, aliishukuru serikali kwa kupeleka miradi hiyo kwa kuwa kilikuwa kilio kikubwa kwa wananchi kupata umeme huku akiahidi kutoa ushirikiano kwa makandarasi ili kufanikisha miradi hiyo.

"Wananchi wana matumaini makubwa na serikali yao hivyo naamini watatoa ushirikiano wa kutosha kwani wamefurahia mno kufikiwa na mradi huu,"alisema.

Mmoja wa wananchi, Hamisi Said wa Kijiji cha Kwahengwa, aliishukuru serikali na kuiomba kwa vile vitongoji ambavyo bado havijafikiwa na huduma ya umeme serikali ivikumbuke.





# Bandari Malindi yazidiwa uwezo katika utendaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Bandari Zanzibar imesema bandari ya Malindi kwa sasa imelemewa uwezo wa upokeaji wa makontena ya mizigo kutokana na mahitaji kuongezeka.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Nahaat Mahfoudh, aliyasema hayo jana wakati mabalozi wa Tanzania wanaoziwakilisha nchi mbalimbali kufanya ziara katika bandari hiyo na ile ya Mangapwani mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema bandari hiyo ilijengwa tangu mwaka 1920 na uwezo wake ni kupokea meli mbili za mizigo lakini kwa sasa mahitaji yameongezeka na kusababisha ufinyu wa nafasi katika bandari hiyo.

"Zamani tulikuwa tukileta makontena 100 bandarini hapa lakini kwa sasa wastani wa makontena 600 tunapokea, hivyo uwezo wa kubeba makontena umeshapitwa na wakati," alisema Nahaat.

Alisema bandari hiyo pia inapitisha watu 5,000 kwa siku kutoka Unguja kwenda Dar es Salaam na kutoka Unguja kwenda Pemba.

Mkurugenzi huyo alisema ugonjwa wa UVIKO-19 umesababisha uingiaji wa mizigo inayotoka nje ya nchi kupungua na gharama kupanda hadi kufika dola 10,000 kutoka dola 3,000 kwa kontena moja kutoka China. Alisema licha ya uchumi kufunguliwa baada ya ugonjwa huo kupungua, bado hali haijarejea kama zamani.

Alisema mamlaka imeagiza mashine za kisasa za kushusha makontena ambazo zitakuwa na uwezo wa kushusha makontena 20 kwa saa moja huku akibainisha kuwa mashine zilizopo ni za kianalojia ambazo hushusha makontena 10 kwa saa moja.

Mashine hizo, alisema zinatarajiwa kufika mwanzoni mwa mwakani na zitaongeza ufanisi wa utendaji kazi bandarini hapo ikiwamo meli za mizigo kukaa muda mrefu bandarini hapo.

Alisema asilimia 95 ya mapato ya mamlaka hiyo yanatoka katika bandari hiyo, hivyo kuimarishwa kwa bandari zingine zilizoko Zanzibar, mapato yataongezeka pamoja na kupunguza msongamano wa abiria na mizigo katika bandari ya Malindi.

Kuhusu ujenzi wa bandari ya Mangapwani, mkurugenzi huyo alisema baada ya kukamilika, itakuwa na uwezo wa kupokea makontena mengi.

Kiongozi mkuu wa mabalozi hao, Dk. Asha Rose Migiro, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kutokana na dira kubwa aliyoiweka kwa maendeleo ya Zanzibar.

"Tutakua na mengi ya kusema tutakapokaa katika kikao lakini niseme tutajadiliana jinsi ya kuzibaini fursa zitakazochochea uwekezaji kwa maendeleo ya Tanzania ikiwamo Zanzibar" alisema.




Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi (katikati), akizungumza na mabalozi wanawake wanaoiwakilisha Tanzania kwenye nchi mbalimbali, walipotembelea katika ofisi ya ZMBF mjini Zanzibar juzi. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

## Wadau wa kilimo, watafiti watakiwa kufanya kazi kwa karibu

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Rasilimali Watu, Utawala na Mipango wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Khalfan Masoud Saleh, amewataka wadau wa kilimo kuwa karibu na watafiti ili kuongeza tija kwenye shughuli zao.

Saleh alitoa rai hiyo wakati akifungua mafunzo yaliyoshirikisha wakulima, mabibi na mabwana shamba yaliyofanyika katika ukumbi wa maabara ya mazao ya nafaka katika taasisi hiyo, Kizimbani Unguja.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwasilisha matokeo ya utafiti wa kuendeleza kilimo bora cha muhogo na viazi vitamu kwa ajili ya kuongeza kipato cha mkulima.

Kwa mujibu wa Saleh, mabadiliko ya tabianchi yamesababisha athari mbalimbali katika kilimo zinazochochea uwepo wa wadudu na maradhi yanayoathiri mazao hayo.

Alisema awali wakulima walikuwa wanapanda na kuweka mbolea bila kufuata au kuzingatia maelekezo wanayopewa na watafiti ambapo sasa tafiti zimeweka miongozo itakayohakikisha mazao hayo yanakua vizuri na endelevu.

Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti, Salma Omar, alisema kuwa mradi huo unahimiza matumizi ya mbegu bora za mhogo na viazi vitamu ili kuongeza uzalishaji sambamba na kujenga uelewa wa matumizi sahihi ya mbolea za viwandani.

Alisema kutokana na kuwapo kwa changamoto zinazowakabili wakulima, wameona umuhimu wa kuwashirikisha maofisa ugani kuandaa mbinu za kuufanya mradi huo uwe endelevu badala ya kuishia katika makaratasi.

"Tunajua mabibi na mabwana shamba ni kiungo kinachowaunganisha wakulima na utaalamu kwenye kilimo hivyo uwepo wenu tunaamini utasaidia maarifa na teknolojia zinazotumika kuwafikia wakulima kuongeza ufanisi katika kilimo chao," alisema Salma.

# SMZ yataka ushirika kuleta maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wadau wa maendeleo, taasisi binafsi, mashirika na jamii kwa ujumla kuendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali ili kuisaidia kufikia malengo yake.

Hemed alisema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya tathmini ya kitaifa ya stadi za maisha iliyofanyika Hoteli ya Verde, Mtoni Zanzibar.

Alisema serikali inachukua jitihada katika kuboresha elimu ikiwamo kufanya tathmini katika sekta hiyo na matokeo yake yanawezesha kuangalia namna bora ya kuimarisha mitaala ya elimu.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inashajihisha wadau wa elimu kuhakikisha wanapata taarifa sahihi za hali ya matokeo ya elimu na makuzi ya Watoto kwa kuzingatia stadi za maisha.

Kwa mujibu wa Hemed, taarifa zilizomo katika tathmini hiyo zitafanya maboresho chanya na yenye tija katika sekta ya elimu kwa lengo la kupata taifa lenye nidhamu, maarifa, ubunifu na kusaidia kupata viongozi bora.

Hemed alitaka jamii kusimamia stadi hizo kwa mustakbali wa vijana na taifa kwa ujumla na kushirikiana katika kuhakikisha stadi hizo zinapewa kipaumbele katika maeneo yote wakiwa nyumbani na shuleni.

Alisema suala la stadi za maisha lina uwanja mpana katika kupunguza umaskini, kufikia usawa wa kijinsia kuhamasisha ukuaji wa uchumi na kutengeneza jamii endelevu na yenye afya na maarifa.

Aidha alieleza kuwa Serikali inategemea nguvu kazi ya vijana wenye maadili mema na wanaojituma ambao uwepo wa stadi hizo za maisha vijana hao wataendana na mahitaji ya karne ya 21.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdul Ghulam Hussein, alisema wizara inaendelea na uandaaji wa mabadiliko katika sekta ya elimu na kwamba uwapo wa mwongozo huo utasaidia wizara kutoa dira ya kukamilisha kazi hiyo.

Mkuu wa Miradi ya Taasisi ya Milele Foundation, Khadija Sharif, alisema wadau mbalimbali duniani wanaendelea kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu ambapo Milele Foundation imeona umuhimu wa kuandaa muongozo huo.


Alisema zaidi ya asilimia 50, Vijana wanaomaliza vyuo hawana ujuzi jambo ambalo limeifanya Milele Foundation ikishirikiana na taasisi zingine kutoka Tanzania, Kenya na Uganda kuona umuhimu wa kuandaa mwongozo huo ili utoe dira ya mageuzi katika sekta ya elimu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**KIBA**
UKURASA 16

JUMAMOSI NOVEMBA 19, 2022



# RAYVANNY

YUKO WAPI ?

# FREDDIE NDALA KASHEBA-1

# Mchawi wa gita 'kombora', akalivunja na kuzikwa nalo

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI Tshala Muana kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mwaka 1994 alirekodi nyimbo mbili zilizojipatia umaarufu mkubwa, 'Kokola' na 'Dezo Dezo.'

Nyimbo hizi alizichukua kutoka kwenye bendi ya Zaita Musica ambazo zote zilitungwa na mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba.

Nyimbo hizi halisi zilirekodiwa kwenye studio za Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na bendi ya Zaita Musica mwanzoni mwa miaka ya 1990, lakini Tshala Muana baada ya kuzichukua yeye alienda kuzirekodia Ufaransa.

Tshala Muana alichukua nyimbo hizi mbili alipokuja nchini miaka hiyo na kufanya ziara, ndipo alipozipenda na kuingia makubaliano na Kasheba, akazichukua.

Hata hivyo baada ya kuona malipo yanachelewa, Kasheba alianza utaratibu wa kushtaki na kuanza kufuatilia malipo yake.

Huyu ndiye Kasheba ambaye pia ni mzaliwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kama Tshala Muana, lakini yeye muziki wake kwa kiasi kikubwa aliufanyia nchini Tanzania ambapo alijipatia umaarufu mkubwa kutokana na utunzi wa nyimbo zake nyingi akiwa na bendi mbalimbali.

Ukiachia hilo, ndiye muasisi wa kupiga gita la solo kwa kutumia nyuzi 12 kiasi cha kuwashangaza wengi, kwani kwa kawaida gitaa hilo hutumia nyuzi sita tu.

Kutokana na utaalam wake wa kuzidonoa nyuzi za gitaa hilo, mashabiki wake wakampachika jina la Maestro, baadhi wanamwita Supreme, pia akaitwa Chunusi, huku gita lake nalo likipachikwa majina mengi kama 'dazeni' kutokana na kuwa na nyuzi 12, lakini pia wapo walioli-batiza jina la kombora, wakiwa na maana jinsi lilivyokaa, muonekano wake ni kama kombora la vitani.

Makala hii inamtazama mwanamuziki huyo maarufu kuwahi kutokea nchini, tangu alipoingia mara ya kwanza na bendi ya Orchestra Fauvette mwanzoni mwa miaka ya 1970, akitokea nchini Zaire (sasa Congo DR), safari yake ya muziki hadi alipofariki dunia 22 Oktoba 2004 jijini Dar es Salaam na kuzikwa kwenye Makaburi ya Kinondoni.



**Kuzaliwa kwake**

Alizaliwa Lubumbashi nchini Congo mwaka 1946 na alianza kufundishwa muziki na baba yake mzazi akiwa na umri wa miaka 12 tu. Pamoja na kwamba hakuwa mwanamuziki, lakini baba yake alijua kupiga gitaa na alikuwa akifanya hivyo nyumbani tu baada ya saa za kazi.

Kila anaporejea kazini na baada ya kupata msosi, anatoka nje na gita lake na kupiga kwa ajili ya kujiburudisha tu, lakini jambo hilo lilimpendeza sana Freddie. Baba yake akaamua kumfundisha jinsi ya kuliadhibu gitaa.

Bendi yake ya kwanza rasmi ilikuwa ni Orchestra Fauvette iliyoandishwa Juni 7, 1964 kwenye jiji la Lubumbashi.

Fauvette walikuwa na maana ya chiriku, kwa sababu bendi ilikuwa na mmoja wa waimbaji ambao wao waliamini kuwa anaimba kama ndege chiriku.

**Kuingia Tanzania**

Baada ya kununuliwa vyombo vipya kabisa aina ya Hofner, bendi ilijiimarisha na kujiamini kiasi cha kufikiria kuondoka nchini mwao kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

Kundi zima la watu tisa akiwemo Kasheba na swahiba wake mkubwa Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki' lilipanda mashua za walanguzi wa chumvi na kuvuka Ziwa Tanganyika toka Congo hadi Tanzania kwa kupitia Kigoma.

Bendi hiyo ilikita makazi yake kwenye ukumbi wa White House, Ubungo ambapo wakati huo ilikuwa mbali na mji, hivyo kulikuwa na ajali nyingi za barabarani ziliwapata mashabiki wa bendi hiyo wakati wa kwenda au kutoka kwenye muziki, hivyo kwa ushauri bendi hiyo ilihama na kukaa kambi kwenye ukumbi wa Mikumi Tours uliokuwa maeneo ya Tazara, Buguruni, wakiporomosha muziki wake siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

# UDAKU TU



# LIMEFUNIKWA

## Rayvanny, WCB kila mtu kivyake

SERIKALI kupitia Baraza la sanaa Tanzania (Basata) limetangaza kumalizika kwa mgogoro kati ya Rayvanny na lebo ya WCB inayomilikiwa na mwanamuziki nyota Diamond Platnumz.

Kauli ya Katibu Mtendaji wa Basata, Dk. Kedmon Mapana wakati akizungumza na Bongo5, inahitimisha mvutano uliokuwa ukifukuta kati ya Rayvanny na mabosi wake wa zamani.

Hata hivyo, utata ulioko katika mkataba uliokuwa unalalamikiwa bado ni siri na haijawekwa wazi kama Rayvanny ametoka moja kwa moja kama ilivyokuwa kwa Harmonize.

Dk. Mapana amesema suala hilo limefunikwa na kila upande sasa uko huru kufanya mambo yake.

Haijafahamika kama Rayvanny amelipa mamilioni ya pesa ili kujitoa WCB, kama alivyofanya Harmonize ambaye ilimbidi kutoa zaidi ya milioni 500.

"Sakata la Diamond na Rayvanny lilikuwa kubwa najua waandishi mlikuwa hamjui linaendaje. Naweza kusema kwamba jambo lao limeisha wasanii wote watafanya kazi zao wakiwa huru," amesema Dk Mapana.

Akaendelea kusema "Rayvanny sasa anafanya kazi zake akiwa huru, kila kitu tumeyafunika, tumeyamaliza kistaarabu,"

Hata hivyo, amewashauri wasanii kuwa makini wakati wanapoingia mikataba katika lebo za muziki, na ikiwezekana kukishirikisha chombo hicho ili kujihakikishia usalama wao.

Dk. Mapana ametoa wito kwa wadau wote katika tasnia ya muziki kufuata taratibu na katiba ili kuondoa malalamiko.

Ameeleza kwenye mikataba kila mtu anaweza kuwa na tafsiri yake, unaweza kuona wa kinyonyaji au wa kibiashara kulingana na maelewano ya watu husika.

"Ni vizuri kupitia mikataba kwanza na kushirikisha baraza kabla mtu hajasaini, wakati mwingine unaweza kumbana na kuuona wa kinyonyaji lakini unaweza ndani ya miaka kumi ukapata faida kubwa na kuona una faida," amesisitiza.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**





**@stevenyerere2**
Ukiwa mpambanaji maishani usikatishwe tamaa na mafanikio ya wapewaji, kwani kuna watu kila walivyo navyo vinatokana na jasho la mtu au watu wengine.

**@masanjamkandamizaj**
HONGERENI WANANCHIIIIIIII. Yaani Hata caption imekataaa ndo maana wanasemaga Tubakizage Maneno.





**@jenniferkyaka**
Kuna nyakati huwa ni za giza kwenye maisha.
Ni kama ndoto zako zinakuwa zimefukiwa na matumaini yamepotea.
Mara nyingi kwenye nyakati hizi, itakuwa kama hakuna mtu anayekujali na umebakia peke yako. Kila unapogeukia kwa ajili ya msaada itakuwa kama hakuna anayejitokeza. Naomba nikukumbushe kuwa, huo ni wakati muhimu sana wa maisha yako na ndoto yako. Ni wakati ambao ndoto yako inajaribiwa ili kuthibitisha kuwa unamaanisha na Uko serious na unachokitafuta. Ukiweza kuvuka wakati huo, utakuwa umeshinda moja ya mitihani muhimu sana kwa maisha yako. Ukivuka hapo, utashangaa kuna ambao ulikuwa unawatafuta wanaanza kukutafuta wao.Nakuombea uwe na nguvu za kuvumilia na kuvuka salama bila kukata tama.

**@hamisamobetto**
Njia pekee ninayoweza kupoteza nafasi yangu ni ikiwa sitaki tena.





**@richmitindo**
Mungu nisaidie nihifadhi hii furaha yangu moja na uniepushe na kujihifadhi na hasada mia moja, nyie hata tukishindia mchunga kwa furaha tuliyonayo tutaiona burger.

BASI SAWA

## Densa aitamani lebo ya muziki



Mcheza shoo wa mziki wa kizazi kipya, anayekuja kwa kasi Hasan Ngole, maarufu kama Ngole The Don, amewaomba wadau kujitokeza kumuunga mkono kupitia kipaji chake ili aweze kutimiza ndoto zake.

Ngole aliliambia BT kuwa ili aweze kutimiza malengo yake anatamani kupata lebo ya mziki itakayomfanya aweze kuonyesha kipaji na anaamini atafanya makubwa ndani na nje ya Tanzania.

"Nina kipaji kikubwa cha kucheza nyimbo yoyote huwa watu wananikodi kwenda kutoa burudani kwenye harusi na matamasha mengine ila kinachoniumiza sina lebo itakayo nifanya nionyeshe uwezo wangu," amesema.

Ngole amesema anataka kuwa Moze Iyobo, anayemilikiwa na lebo ya Wasafi, kama akipata sehemu ya kukuza kipaji chake.

## Madee amkubali Kontawa



RAIS wa Manzese Music Baby (MMB) Madee amesema msanii anayekuja kwa kasi Kontawa, anatakiwa kuangaliwa kwa umakini kutokana na kazi yake nzuri.

Kontawa ambaye anatamba na ngoma yake 'Champion' ameelezewa kama msanii wa kuzingatiwa mwaka 2023.

Kupitia lebo yake ya MMB Madee tayari ameshatoa wasanii kadhaa kama Dogo Janja, Maarifa na Gazza.



## GIGY MONEY HAMTAKI MTOBOA PUA

MWANAMUZIKI Giggy Money, amesema kamwe hawezi kulala kitanda kimoja na mwanaume aliyetoboa.

Akizungumzia kitendo cha msanii Diamond Platnumz kutoboa pua, Giggy amesema hawezi kumzungumzia msanii huyo, lakini kwake hataki kumuona mwanaume wake anafanya jambo hilo.

"Diamond kamaliza starehe zote na sasa kaamua kutoboa pua, huo ni uamuzi wake lakini kwangu sitaki mwanaume wangu kutoboa pua halafu tulale kitanda kimoja, hilo halitawezekana," amesema Giggy.



## Kiba azidi kuwasha moto Marekani

MWIMBAJI na bosi wa lebo ya Kings Music, Ally Salehe Kiba, almaarufu Alikiba anaendelea kuwasha moto nchini Marekani katika ziara yake ya kimuziki.

Kiba yupo nchini humo kuwatumbuiza mashabiki wake katika ziara hiyo ya kutangaza albam yake ya 'Only One King' ambayo itamfikisha katika majimbo mbalimbali nchini humo.

Wiki hii amefanya shoo kwenye miji miwili na ataendelea kupanda jukwaani katika miji mingine na kufikisha 10.

## WASAUZI WA KIKE WALIOTAMBA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

TANGU enzi za ubaguzi wa rangi, nchini Afrika Kusini kumekuwa na wanamuziki wengi mahiri kubahatika kutamba ndani na nje ya nchi hiyo.

Kwa bahati ni kwamba wanamuziki wengi mastaa Sauzi ni weusi, ambao walifanya kazi kubwa tangu enzi za kudai uhuru hadi ulipopatikana.

Wakaendelea na maisha ya muziki, lakini wakajitokeza wengi wazuri zaidi.

Kifupi tu ni kwanza Sauzi haijawahi kukaukiwa na wanamuziki mahiri na wenye viwango vya hali ya juu.

Hapa nchini mbali na kuwapokea wapigania uhuru, lakini pia ilipokea baadhi ya wanamuziki wakawa wanapiga bendi mbalimbali kabla ya nchi zao kupata uhuru na kuondoka.

Leo hii tunawaangalia wanamuziki wa kike tu ambao walipata kutamba Afrika nzima, wakijipatia mashabiki wengi nchini Tanzania kutokana na nyimbo zao.

**Miriam Makeba**

Huyu anaitwa mama Afrika. Alizaliwa mwaka 1932 na kufariki dunia 2008 bado akiwa mwanamuziki.

Ni mmoja wa wanamuziki maarufu si Afrika tu bali dunia nzima. Alianza kuimba nyimbo zake wakati ule wa ubaguzi wa rangi na zikavuma sana, zikawa maarufu hadi leo hii.

Baadhi ya nyimbo zilizompatia umaarufu mkubwa ni kama 'Patapata', 'Hapo Zamani', 'Malaika', "Welela', 'Soweto Blues' na nyingine nyingi ambazo zilikuwa na mashabiki wengi nchini.

**Doroth Masuka**

Unaweza ukasema kama huyu ni pacha ya Miriam Makeba. Naye alizirudia nyimbo za 'Patapata' na 'Hapo Zamani'. Pia kuna utata kwani inasemekana huenda Doroth ndiye mtunzi halisi wa wimbo wa 'Hapo Zamani' ana uraia wa Zimbabwe na Afrika Kusini pia. Alishawahi kuja nchini miaka ya 1960 na kupigia bendi mbalimbali nchini, akarekodi nyimbo mbili kwa kiswahili kama 'Kunguni' na 'Viongozi Afrika'. Alirejea Sauzi na kuendelea na mambo yake ya muziki akirekodi nyimbo mbalimbali hadi alipofariki nchini Afrika Kusini mwaka 2019.

**Yvonne Chakachaka**

Kizazi cha miaka ya 1980 wanamkumbuka mwanamuziki huyu kwani ndiyo kipindi chao cha utoto wakati nyimbo zake zinazuma.

Umaarufu wake ulianza katikati ya miaka ya 1980 alipotoa albamu yake iitwayo 'Thank You Mr DJ' ya mwaka 1987 ambayo si tu kwamba ilimtoa ikiwa pia na wimbo mwingine maarufu 'Umqombothi', lakini ndiyo kama vile alifungulia maji kwenye koki.

Baada ya hapo alianza kutoa ngoma mfululizo kama vile 'Sangona', 'Bombani', 'I Cry For Freedon' na nyingine nyingi.

**Brenda Fassie**

Mwanamuziki huyu aliyezaliwa mwaka 1964 na kufariki 2004 alikuwa mmoja wa wanamuziki wa kike wa Sauzi waliopendwa sana nchini Tanzania.

Na hasa alipotoa ngoma yake ya 'Vulindlela' ambayo ilikamata sana Bongo kiasi cha yeye mwenyewe kuja nchini na kufanya maonyesha kadhaa. Na alipondoka kurudi kwao alitunga wimbo 'Nakupenda' alioimba kwa lugha ya kiswahili.

**Pamela Nkuta**

Ni mwanamuziki ambaye alipata sifa kwa muda mfupi tu hapa nchini kutokana na wimbo wake uitwayo 'Melody' ambao ulikuwa na sauti ya mtoto analia wakati wimbo huo unaanza na yeye mwenyewe kuimba kama vile anambembeleza.

FILAMU

## Kipofu: Kuwa makini, usimdharau binadamu

**Na Adam Fungamwango**

KANUNI kuu ya majasusi na wapelelezi ni kutomuamini mtu yeyote Yule, kutomdharau yeyote Yule na kuwa makini na kitu chochote kile hata kama ni maiti. Yako mengi sana, lakini haya niliyoyaainisha yanatosha kwa muktadha huu ninaotaka kuuandika hapa.

Naileta kwenu filamu moja matata sana iitwayo Kipofu. Ifuatilie hadi mwisho utaamini kile ambacho ninakisema na nadhani kuna kitu utajifunza.

Waliocheza ni Elia Daniel, Yasmine, Ummy Hellen, Subira Mohamed na wengineo.

Filamu inamuonyesha kijana mmoja aiitwaye Kilonzo akiwa amekaa sehemu moja hivi akiwa anapunga upepo na mpwa wake Yasmine.

Kilonzo ni kijana kipofu ambaye alipanga chumba maeneo hayo, lakini akiwa na msichana mmoja ambaye ni mpwaye.

Yasmine ndiye anayemsaidia mjomba wake kwa kila kitu, kumtembeza kwenda kuomba mjini, kumpikia na kila kitu. Kifupi anaishi naye hapo na yeye ndiye kama macho yake.

Wamepanga chumba kimoja tu, lakini jirani hapo kuna mti moja wenye kivuli ambao hupenda kukaa na mpwaye.

Mkabala na sehemu hiyo na jumba kubwa mithili ya hekalu.

Tabia yao ya kwenda kuombaomba inawakera baadhi ya watu ambao wanawaletea maneno machafu, kuwatukana na maneno ya dharau.

Siku moja wanaamua kwenda kuomba kwenye jumba hilo kubwa lililo mkabala na hapo wanapopenda kukaa chini ya mwembe. Mama mmiliki wa jumba hilo anatoka na kuanza kuwatolea maneno ya shombo.

Mbali na kuwazodoa anamwambia Yasmine kuwa yeye ni mrembo, hivyo anaweza kutumia uzuri alionao kumlisha mjomba wake badala ya kuombaomba.

Nyumba ya sehemu ambayo hupenda kubarizi kuna dada mmoja mrembo



anaitwa Malkia. Mara kwa mara humsikia akiwatukana kwenye simu na kuwabeza wanaume, lakini pia akionekana kuwakomoa kwa kuwaomba pesa.

Kilonzo siku moja akamtolea uvivu na kumpasha laivu kuwa asitumie urembo wake kuwafanya wanaume mtaji.

Hata hivyo alikumbana na maneno ya kashfa kutoka kwa Malkia, kadri muda ulivyozidi kwenda ni kama maneno yale yalikuwa yakimuingia. Kuna siku alikwenda nyumbani kwao na kumuomba radhi. Akamwambia aliathirika na kuwachukia wanaume kutokana na kutendwa.

Baada ya hapo Kilonzo akawa na uhusiano mzuri na Malkia, huku akiwakaribisha nyumbani kwake mara kwa mara yeye na Yasmine kwa chakula cha mchana.

Siku isiyo na jina, askari polisi wanavamia nyumba ya mwanamama mwenye hekalu mkabala ya eneo ambalo Kilonzo na Yasmine walipenda kwenda kukaa.

Mama huyo anatiwa mbaroni kwa kujihusisha na madawa ya kulevya. Alikamatwa na mzigo mkubwa ambao kesho yake alikuwa ausafirishe nje ya nchi. Waliofanikisha kukamatwa kwake ni Kilonzo na Yasmine. Kumbe hakuwa kipofu. Alijifanya hivyo kwa ajili ya kuichunguza nyumba ile, na kupenda kukaa pale ni kwa ajili ya kuangalia mwenendo na kupiga picha kila kinachofanyika.

Walipomaliza kazi yao walikwenda kumuaga Malkia. Alipatwa na furaha mshtuko kuona kumbe Kilonzo hakuwa kipofu.

Jina lake halisi ni Mr David, akaamua kujiita Kilonzo. Yeye na Yasmine walikuwa ni askari wapelelezi.

BONGO FLEVA

# TUTAWABANA WATAACHIA TU



MSANII anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Starshine TZ ametamba kutokana na hali inavyokwenda na kusema ufahari wa wasanii wachache utafika ukingoni.

Amesema kwa sasa kuna vipaji vipya akiwemo yeye wanakuja kwa kasi na kuhitimisha utawala wa mastaa wa muziki nchini Diamond,Harmonize na Ali Kiba.

Amesema katika kipindi kifupi tangu aingie kwenye muziki, mashabiki wamempokea kwa nguvu kutokana na ngoma kali alizoziachia.

"Unajua vipaji vipya vinakuja kwa kasi, kila siku tunatoa ngoma nzuri inayotishia utawala wa watu, natumaini tutakuwa na wasanii wengi wenye mafanikio kama nchi nyingine," amesema Starshine tz.

Amesema ataufunga mwaka kibabe kwa kuachia ngoma tatu mfululizo zenye ladha tofauti ili kukata kiu ya mashabiki.

Starshine amesema ngoma hizo zitakuwa katika mahadhi ya Bongo Fleva, Singeli na Amapiano huku akizingatia ubora wa muziki wake ili kuleta ushindani kwenye soko.

"Nina ujio wa ngoma tatu kwa mpigo kabla ya mwaka kuisha ambazo ni Amapiano, Bongo Fleva na Singeli, zitakuwa kwenye ushindani wa levo za kina Diamond, Harmonize na Alikiba hivyo mashabiki wakae mkao wa kusikiliza," amesema Starshine.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**

Kila siku ya Jumamosi kama leo kundi zima la wana Ngwasuma chini la Patcho Mwamba, hufanya vitu vyao katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, uliopo kando ya Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam.

**Tukuyu Sound Band**

Kila Jumapili vijana wa bendi hii huwa wanamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma

Orchestra Sikinde Original

Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Becah, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Waluguru Original**

Kama kawaida, bendi hii ya mjini Morogoro, kila Jumamosi hufanya vitu vyake katika ukumbi wa Terminal Pub Msamvu na Jumapili itakuwa ndani ya ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

**Town Classic Band**

Jana walikuwa ndani ya ukumbi wa Andrews (zamani T-Garden) Sinza, leo watakinukisha katika ukumbi wa Buga Lounge Kimara Korogwe, Jumapili wapo ukumbi wa Kibozone Malamba Mawili Mbezi.

**Kimokimo Band**

Wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Maina Band**

Bendi hii inayoongozwa na mwimbaji mkongwe, Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.

**Twanga Pepeta**

Kila Ijumaa huwa wanatoa burudani ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, kesho Jummpili watamalizia wikiendi katika wa Gwambina Lounge, zamani TCC Club Chang'ombe.



# WENZAO WANAJAZA KUMBI MAARUFU, WAO WANAPIGANA MAJUNGU BONGO

WASANII wa Tanzania wanajisifia kwa kuwa na maisha ya kifahari, kuendesha magari na majumba ya kisasa.

Kila kukicha wanatupiana maneno ya kukejeliana na kusababisha mitafaruku isiyo na maana kwa wafuasi wao na kuacha nyuma jukumu lao la kisanii.

Lakini kwa Wanigeria wao ni tofauti, kwa sasa wapo katika vita kushindana nani anaweza kuvunja rekodi ya kujaza kumbi maarufu duniani kama walivyofanya wasanii wa kimataifa.

Wakati wasanii wetu wa Bongo wao wanajigamba kwa kujaza watu katika kumbi za baa wanapofanya ziara nchini Marekani, Wizkid yeye anafurahia kuujaza ukumbi maarufu nchini humo Madson Square Garden kama walivyofanya wasanii wachache wakubwa duniani.

Wizkid anaungana na Michael Jackson, Elvis Presley, The Beatles, Adele, Rihanna, Jay-Z, Justin Bieber na Mariah Carey, kwenye orodha ya wanamuziki ambao wamewahi kuujaza ukumbi huo ulioko katika jiji la New York.

Ukumbi huo wenye umaarufu zaidi duniani, una uwezo wa kuingiza watu 20,789 kwa wakati mmoja.

Kwa bara la Afrika hakuna msanii wa Afrika Mashariki aliyefanikiwa kujaribu wala kufikiria kunusa ukumbi huo, lakini The African Giant, Burna boy naye alifanikiwa kuujaza.

Wengi huamini Wanigeria ni wengi duniani na ndio husaidia kujaza shoo za wasanii wao kwenye mataifa makubwa ya Kiburudani kama Marekani, Uingereza, Ufaransa na mataifa mengine.

Hata hivyo, hoja hiyo inakuwa butu kwa wadau wa muziki ambao wanasema kila kizuri lazima kinajiuza. Wasanii wa Bongo hakuna hata mmoja anayefikiria jambo hilo, badala yake wanaendelea kupigana mikwara isiyo na tija.



# Rejoice hongera kuuaga ukapera

IMEKUWA wazi sasa Rejoice Iwueze, mwimbaji mkuu wa Destined Kids, amefunga ndoa na rafiki yake wa zamani.

Msanii huyo alichapisha picha zake na mwenzi wake wakiwa wamevalia mavazi ya kitamaduni kwenye mitandao ya kijamii baada ya sherehe ya harusi yao iliyofanyika juzi.

Awali Rejoice aliweka picha kwenye ukurasa wake wa Instagram akionyesha pete yake ya uchumba, kisha kuweka ujumbe mzito ambao ulimsifia mpenzi wake Samuel.



## Chinko ilikuwaje ukatapeliwa?

RAPA wa Nigeria, Oladipo Emmanuel maarufu kama Chinko Ekun, inadaiwa amefilisika kiasi ambacho amekosa makazi ya kuishi.

Msanii huyo ambaye alikuwa chini ya Olamide Badoo, imeelezwa amepatwa na mkasa wa kufilisika baada ya matapeli wa uwekezaji kumsababishia kupoteza mamilioni ya pesa kwa ofa za uwongo.

Katika mazungumzo na Midweek Entertainment, mwimbaji huyo wa wimbo wa Able God alifichua kuwa tukio hilo la kusikitisha lilibadili mtazamo wake wa kuwekeza na kuwa maskini.

## Crayon mambo ya ndani ni siri

WATUMIAJI wa mitandao wamejikuta wakitaharuki baada ya ujumbe tata kutoka kwa mwimbaji chipukizi wa Afrobeats Charles Chibueze Chukwu, maarufu kama Crayon.

Crayon, msanii kutoka lebo ya Mavin Records, hapo awali alitweet kuhusu uzoefu wake na baadhi ya mambo ya kwanza aliyojaribu baada ya kusaini mkataba wa rekodi.

Crayon alidai kwamba kila kitu alichojaribu kwa mara ya kwanza kilikuwa cha kushangaza, ikiwamo kufanya mapenzi kwenye baa.





## Card B asimulia mumewe anavyolia

MWANAMUZIKI maarufu wa Marekani Cardi B, ambaye ameolewa na rapa Offset, amefichua kuwa mume wake bado anaamini rafiki yake Takeoff, bado yuko hai.

Cardi B, amesema kuna barua za mume wake ambazo ameziandika kwa hisia kali huku akieleza bado haamini kama kifo kimemchukua mwanamuziki huyo.

"Moyo wangu umevunjika na nina mambo mengi ya kusema, lakini siwezi kupata maneno. Nimekuwa nikienda kulala na kutumaini kwamba yote haya ni ndoto, lakini ni ukweli, na ukweli unahisi kama ndoto mbaya." Moja ya barua hiyo ilisema.

## Duh! Portable kidume cha mbegu

MWIMBAJI mwenye utata, Habeeb Okikiola, almaarufu Portable, ameibua mjadala baada ya kuwapa ujauzito wanawake wawili kwa mpigo.

Hata hivyo, Portable imeelezwa mwanamke wa pili ndiye anataka kumuoa na hivi karibuni wataenda kanisani kula viapo.

Chanzo kilicho karibu sana na mwimbaji huyo kilithibitisha tukio hilo kufuatia ripoti zilizoibuka wiki moja kwamba Portable alimpa ujauzito mwanamke huyo na kumtambulisha kwa mkewe Bewaji.



**MAKALA**

# Kenyatta kuutafuna mfupa ulioshindikana?

## • Alichoshuhudia Goma kinatosha

**Na Mwandishi Wetu**

MGOGORO kati ya nchi mbili wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda unazidi kupamba moto na kutishia uwepo wa vita kamili.

Katika hali hiyo ya wasiwasi, waasi wa M23 wanatajwa kama chanzo kikuu kutokana na kuanzisha mapigano mapya na kuteka baadhi ya maeneo mashariki mwa DRC.

Nchi ya DRC inaituhumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi hao na kuwapatia silaha, lakini Rwanda inakanusha Kutokana na kuwepo na mvutano huo mkali ambao unatishia nchi hizo kuingia vitani, Rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta, ameteuliwa kuwa msuluhishi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na tayari ameanza kufanya kazi hiyo.

Katika hatua ya kwanza, Kenyatta aliitisha mkutano wa pamoja kati ya vikundi vya waasi na serikali kujadili amani, huku wakiwatupa nje M23 kwa kile kinachodaiwa ni kikundi cha kigaidi.

Hatua ya pili ni kulipeleka jeshi la kikanda ambalo litakuwa na majukumu ya kupambana na waasi, tayari Kenya imeanza kuwapeleka wanajeshi wake katika jimbo la Goma kuungana na wanajeshi wa Burundi.

Katika kuonyesha, jukumu hilo analifanya kwa ukamilifu Kenyatta, wiki hii alikwenda Goma na kuangalia hali halisi katika eneo, huko amekwenda hadi eneo la Kibumba, umbali wa kilomita 20 kaskazini mwa Goma ambako maelfu ya raia wamekimbia kutokana na mapigano.

Kibumba inachukuliwa kuwa moja ya vikwazo vya mwisho kwa waasi hao kabla ya kufika Goma, ambao ni mji wa kibiashara unaokaliwa na watu milioni moja ambao uko kwenye mpaka na Rwanda.

Kabla ya kuwasili eneo hilo, kulikuwa na uvumi ulioenea kwamba M23 walikuwa wanakaribia, na kusababisha wimbi jipya na watu kukimbilia kambi ya Kanyaruchinya, kusini mwa Kibumba.

Takribani watu 40,000 wanaishi kambini hapo kwa sasa, kulingana na mkuu wake.

Ofisa wa usalama ambaye hakutaka jina kuwekwa wazi anasema watu walianza kukimbia baada ya kuona wanajeshi wa DRC wakirudi nyuma kuelekea Goma baada ya makabiliano na waasi wa M23.

Gavana wa kijeshi wa mkoa wa Kivu Kaskazini, Jenerali Constant Ndima, aliwahimiza watu kusalia watulivu akidai vikosi vya serikali vinadhibiti.

"Nataka kuwahakikishia vikosi tiifu kwa serikali vinamdhibiti adui katika milima ya Kibumba," aliwaambia waandishi wa habari.

Mzozo huo umevuruga uhusiano kati ya DRC na jirani yake mdogo zaidi Rwanda.

**SIWEZI KUPUUZA**

Uhuru Kenyatta, alipotembelea kambi ya wakimbizi ya Kanyaruchinya, aliwaambia waandishi wa habari kwamba simulizi alizozisikia zilikuwa zinavunja moyo.

"Siwezi kupuuza nilichokiona," Kenyatta alisema. "Lazima niseme kwa pande zote hamuwezi kujadili katikati mwa janga la kibinadamu" alikemea.

Ziara ya Kenyatta nchini DRC ameifanya kama juhudi zake za kidiplomasia kutatua mzozo katika eneo tete la mashariki mwa nchi hiyo maskini.

Rais huyo wa zamani wa Kenya, baada ya kujionea hali halisi alikwenda mji mkuu wa Kinshasa kwa ajili ya mazungumzo na Rais Felix Tshisekedi.

Mkutano kama huo umefanywa na rais wa Angola Joao Lourenco, lakini bado haujaonyesha mafanikio.

Hata hivyo, mazungumzo mengine yanayofadhiliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki yameitishwa katika mji mkuu wa Kenya Nairobi Novemba 21 mwaka huu.

**KIKOSI CHAWASILI**

Wanajeshi wa Kenya waliwasili mjini Goma mwishoni mwa wiki, kama sehemu ya operesheni hiyo.

Licha ya hatua hiyo, Kenyatta aliyahimiza makundi yenye silaha kuweka chini silaha zao na kurejea kwenye meza ya mazungumzo.





"Hakuna kinachoweza kupatikana kupitia mtutu wa bunduki," aliwaambia waandishi wa habari.

**MAREKANI YAJITOKEZA**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, alisema alizungumzia hali ya nchini Congo na waziri wa mambo ya kigeni wa Rwanda Vincent Biruta, kandoni mwa mkutano wa kilele wa kundi la mataifa G20 nchini Indonesia.

"Nilitiliza mkazo wasiwasi mkubwa wa Marekani kuhusu kuendelea kwa vurugu mashariki mwa DRC, na kuitolewa wito Rwanda kuchukuwa hatua kuwezesha kupungua kwa vurugu," aanasema katika ujumbe wa twitter.

Biruta, kwa upande wake, alitweet kwamba Rwanda imejifunga kwenye mifumo ya kidiplomasia ya kanda inayokusudiwa kuleta amani mashariki mwa DRC.

Zaidi ya makundi 120 yenye silaha yanarandaranda kwenye kanda hiyo, mengi yakiwa urathi wa vita vya kikanda vilivyopamba moto mwishoni mwa karne iliyopita.

**KUIBUKA UPYA M23**

Kundi la M23 ambalo enye wapiganaji wengi wa jamii ya Watutsi lilianza kupata umashuhuri mwaka 2012, baada ya kuuteka kwa muda mji wa Goma kabla ya kufurushwa na vikosi vya Umoja wa Mataifa.

Lakini kundi hilo lilirejea mwishoni mwa 2021 baada ya miaka kadhaa ya diplomasia, likidai DRC imeshindwa kutimiza ahadi ya kuwajumuisha wapiganaji wake kwenye jeshi la taifa.

Awali liliteka mji wa kimkakati wa Bunagana kwenye mpaka wa Uganda mnamo mwezi Juni.

Katika wiki za karibuni, waasi hao wamepata ushindi kadhaa dhidi ya jeshi la Congo, na kusogea karibu kuelekea Goma.

DRC ilimfukuza balozi wa Rwanda mwishoni mwa mwezi Oktoba katikati mwa mashambulizi mapya ya M23. Licha ya ukanushaji rasmi kutoka Rwanda.

Hata hivyo, Rwanda inaituhumu serikali ya Congo kwa kula njama na wapiganaji wa Kihutu waliokimbilia nchini humo baada ya mauaji ya kimbari ya Rwanda mwaka 1994. **DW**




MAKALA

# Saratani ya korodani tishio

## • Wanaume mil. 1.41 wafariki dunia mwaka huu

Na Mwandishi Wetu



Korodani yenye saratani

KORODANI ni moja ya kiungo katika mfumo wa uzazi kwa wanaume.

Kiungo hiki kinapatikana chini ya kibofu cha mkojo na kazi yake kubwa ni utengenezaji majimaji ambayo hubeba mbegu za kiume za uzazi.

Majimaji haya ni muhimu kwa ajili ya uhifadhi na ukuaji mbegu za kiume.

Hata hivyo, korodani inaweza kuathiriwa na magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani.

Saratani ya korodani imeanza kuwa miongoni mwa magonjwa hatarishi kwa wanaume duniani kote.

Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa, iliyotolewa mwezi Machi, 2022, saratani ni ugonjwa unaoongoza duniani kwa kusababisha idadi kubwa ya vifo, huku watu milioni 10 wakifariki dunia kutokana na saratani mwaka huu pekee.

Idadi hiyo ni sawa na kifo kimoja kati ya vifo sita.

Kulingana na ripoti hiyo, watu milioni 1.41 walifariki kutokana na saratani ya korodani.

Kwa mfano nchini Marekani taasisi ya kukabiliana na saratani inayofahamika kama American Cancer Society (ACS) inakadiria kuwa wanaume wapya 268,490, watakuwa wamepatikana na saratani hiyo ndani ya mwaka huu.

**SARATANI INATOKEAJE?**

Saratani ya korodani hutokea pale ukuaji wa seli zisizo za kawaida unapojitokeza katika tezi ya korodani na hali hii huwatokea wanaume pekee.

Kwa kawaida homoni za testosterone hudhibiti utendaji wa korodani ambayo hutengeneza majimaji , yanayofahamika kama 'semen' kwa lugha ya kitaamu.



Semen huwa ni mbegu za kiume za uzazi ambazo hutoka nje kupitia mrija wa mkojo wakati mwanaume anapomaliza tendo la kujamiiana.

Wakati ukuaji usio wa kawaida wa tezi ndani ya korodani unapotokea, ukuaji wa seli mbaya pia huongezeka na hali hiyo huitwa uvimbe ambao hutokea katika korodani.

Kwa sababu saratani hutengenezwa na seli kutoka katika korodani, hapo ndipo huitwa saratani ya korodani.

Saratani hii inaweza kusambaa kwenye maeneo mengine ya mwili .

**KUGUNDUA MAPEMA**

Dk Afred Karagu (Pichani) anasema, saratani ya korodani ni mojawapo ya ugonjwa unaowapata wanaume zaidi, lakini ni pia ni saratani inayoweza kupona iwapo itagundulika mapema.

Mtaalamu huyo wa magonjwa ya saratani kutoka Rwanda anasema njia mojawapo bora zaidi za kugundua saratani hiyo hata kabla ya dalili yoyote kujitokeza ni kwenda kufanyiwa uchunguzi.

''Kadri inavyogundulika mapema kuwa una saratani ya korodani , ndivyo inavyoweza kuwa rahisi kutibika.", anasema Dk. Karagu.

Anasema saratani ya korodani ina uwezekano mkubwa wa kutibiwa na ikapona kabisa iwapo itagundulika mapema.

Hatahivyo anatahadharisha kuwa saratani ya korodani inapochelewa kugundulika, inaweza kuwa imesambaa kwenye maeneo mengine ya mwili au viungo vingine vya mwili na kuleta hatari ya kupoteza maisha.

"Ikifikia katika kiwango hicho huenda isitibike na ndio maana tunahimiza kuwa wanaume watu wazima ni vyema wakafanya uchunguzi wa mara kwa mara wa afya zao , ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya korodani. '' anasema.

Saratani ya korodani pia imewekwa katika makundi mawili kulingana na kasi ya ukuaji wake. Kuna saratani ya korodani inayokua kwa kasi (aggressive) na ile ya korodani isiyokuwa haraka (nonaggressive).

**SARATANI NA TENDO LA NGONO**

Daktari Karagu anasema saratani ya korodani haihusiani na tendo la ndoa, badala yake kuna imani ambazo sio za kweli kwamba watu wakifanya tendo la ngono sana hawawezi kupata saratani ya korodani.

"Hilo si kweli hata unapofanya tendo hilo kila mara unaweza kupata saratani ya korodani, hizi imani sio za kweli '', ameiambia BBC

Aina ya saratani ya korodani ambayo haikui haraka, uvimbe wake hukua taratibu, hata hivyo saratani ya korodani inayokua kwa kasi, uvimbe wake hukua kwa kasi na inaweza kukua kupita kiasi na kusambaa katika maeno mengi ya mwili.

Usambaaji unaweza kuenea kwenye mifupa hali inayojulikana kama saratani ya metastatic.

**DALILI ZAKE**

Kulingana na Dk. Karagu, zipo dalili mbali mbali za saratani ya korodani miongoni mwake ni kuhisi ugumu katika kukojoa, damu katika mkojo, upungufu wa nguvu za kiume,maumivu ya mifupa, maumivu ya tumbo na kupungua kwa uzito wa mwili.

> **"Ikifikia katika kiwango hicho huenda isitibike na ndio maana tunahimiza kuwa wanaume watu wazima ni vyema wakafanya uchunguzi wa mara kwa mara wa afya zao , ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya korodani. " anasema.**

**NANI ANAWEZA KUPATA?**

Walio kwenye hatari ya kupata tatizo hilo ni mwanaume wenye umri wa kuanzia miaka 40 na kuendelea.

Watu wenye umri huo wanatakiwa kufanya uchunguzi wa afya zao wa mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya korodani.

Hatahivyo anashauri kuwa wanaume wenye umri wa kuanzia miaka 50 wanakabiliwa na uwezekano mkubwa wa kupatwa na saratani ya korodani zaidi hivyo basi wanashauriwa kuhakikisha wanapimwa haraka.

Pia walio kwenye hatari ya kupata saratani hiyo ni watu wenye asili ya Kiafrika, watu wenye historia ya matatizo hayo, wenye uzito wa kupindukia, unywaji wa pombe wa kupindukia, ulaji wa nyama nyekundu na ulaji wa vyakula vyenye mafuta mengi

**UNAWEZA KUJILINDA?**

Dk. Leo Ngeruka anasema mambo yafuatayo yanaweza kusaidia kupunguza uwezekano wa kupata saratani hatari ya korodani.

Katika kujilinda zaidi watu wanatakiwa kuimarisha uzito wa mwili, kufanya mazoezi ya mara kwa mara, kula mlo kamili hasa matunda na mboga, kupunguza ulaji wa nyama nyekundu na mafuta.

**Chanzo: BBC**

# Simulizi zinazohuzunisha

## • Baraka za mapacha zinapoleta upweke

Na Sabato Kasika



WAKATI akiwa na ujauzito wa miezi mitano, Monica Marko (24) ambaye pia ni mlemavu wa upofu, anajikuta akipata pigo la kukimbiwa na mwanamume aliyempa ujauzito, akidai hawezi kuwa na mtoto na mtu mwenye ulemavu wa kutoona.

Pamoja na kauli hiyo iliyompa machungu, lakini Monika hakukata tamaa, alilea ujauzito wake kwa taabu na mashaka mpaka alipojifungua salama watoto wake mapacha.

Akizungumza na Nipashe wakati wa ziara ya Taasisi ya Eden Twins Foundation, jijini Dar es Salaam, Monica anasema alikuwa na wakati mgumu kupambana na hali hiyo ambayo kwake kutokana na ulemavu wa macho alishindwa kumudu kazi nyingi.

Taasisi hiyo ilifanya ziara hiyo kwa ajili ya kuwapa msaada wazazi na familia zenye watoto mapacha zisizo na uwezo kiuchumi.

Monica ni miongoni mwa wazazi wenye watoto mapacha wenye mwaka mmoja na miezi miwili sasa, anaishi eneo la Saku, Chamazi ambako taasisi hiyo ilifika kumpa msaada ukiwamo wa vyakula, nguo, sabuni na vitu vingine.

Ilikuwa ni Novemba 11 ambapo taasisi hiyo imeitenga kama maadhimisho ya Siku ya Mapacha, ambapo inazungukia familia kadhaa na kutoa msaada ili angalau kuzipumguzia ukali wa maisha.

"Mimi nimepata ulemavu huu nikiwa darasa la sita nyumbani kwetu Singida, hivyo kama hujafa, bado hujaumbika. Niliumia sana huyu aliyenipa mimba kudai kwamba hawezi kuzaa na kipofu,"anasema Monica.

Huku akilengwalengwa na machozi, binti huyo anasema wazazi wake walijitahidi kwa hali na mali kumtafutia matibabu, lakini dawa alizotumia hazikumsaidia kurudi katika hali yake ya zamani.

### MAISHA YAKE

Monica anasema kwa sasa hana shughuli yoyote ya kumwingizia kipato, bali anaishi kwa kusaidiwa na wasamaria wema ikiwamo taasisi hiyo ambayo inamlipia kodi ya chumba alichopanga.

"Kama nikiwezeshwa kupata cherehani, ninaweza kushona nguo na kujiingizia kipato, kwani ninajua kushona kwa kutumia hata hizi cherehani za kawaida ambazo watu wengine wanaoona wanatumia," anasema.

Anasema akipata cherehani hiyo inaweza kumsaidia kumpunguzia utegemezi, kwa madai kwamba hawezi kuufanya ulemavu alionao kuwa kitegauchumi, badala yake anataka kuonyesha si kigezo cha kutojishughulisha.

**"Taasisi yetu inajishughulisha na msaada kwa familia zenye watoto mapacha zisizo na uwezo.Kwa miaka miwili ambayo tumefanya kazi hii tumebaini mengi, ndio maana tunashauri waingizwe katika kundi maalum," anasema.**

"Nina mdogo wangu wa kiume ambaye ananisaidia katika ulezi wa hawa watoto, hivyo nikipata cherehani, anaweza kuwa anakaa nao huku mimi nikiendelea na shughuli za kuniingizia kipato," anasema.

### HAWA NAYE YAMKUTA

Hiki ni kisa kingine cha Victoria Genes, mama wa mapacha watatu anayeishi eneo la Maji Chumvi Tabata Kisukuru Dar es Salaam, ambaye anasema alikimbiwa na mzazi mwenzake baada ya kujifungua mapacha watatu.

Kwa sasa watoto hao wana umri wa miezi tisa, wakilelewa na mama yao huyo anayejishughulisha na biashara ya mama lishe ili kujikimu kimaisha na watoto wao hao watatu na wengine wakubwa wawili.

"Wa kwanza kama mnavyomuona ana tatizo kidogo la mtindio wa ubungo na anayemfuata ni mzima, hawa baba yao ni mwingine, wote ninawalea mwenyewe, bila msaada wowote," anasema Victoria.

Anasema kulea mapacha watatu ni kazi kubwa bila kupata msaada upande mwingine, na kwamba kama baba yao angekuwepo, wangesaidiana, lakini akamwachia na kwenda kusikojulikana.

"Tangu alipoondoka wakati nimejifungua, alibadili namba ya simu simpati tena na sijui yuko wapi. Ukweli ni kwamba tulikutana tu hapa jijini na kuwa marafiki, akanipa ujauzito, lakini akanikimbia kwa kuzaa mapacha," anasema.

Naye Grace Ngoje mama mzazi wa mapacha watatu wenye umri wa mwaka mmoja, mkazi wa Buguruni Dar es Salaam, anasema alikimbiwa na mzazi mwenzake na kuambiwa kuwa kuzaa mapacha ni uchuro.

"Mzazi mwenzangu alisema kwao hakuna mapacha, na kwamba nisimletee uchuro, bahati nzuri nimeendelea kuwalea mwenyewe nikisaidiwa na watu wema, na sasa watoto wamefikisha mwaka mmoja," anasema Grace.

Anasema mwanzoni alipokimbiwa, alitamani kuwatupa watoto hao, lakini akapata ushauri nasaha kutoka kwa mwenyekiti wa taasisi hiyo na kubadili mawazo na kuamua kulea watoto wake hao.

### OMBI SERIKALINI

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Diana Mbena, anasema ni vyema familia za watoto mapacha zisizo na uwezo zikatambuliwa na kuwekwa katika kundi maalum ambalo litafuatiliwa kwa karibu na kutatuliwa changamoto.

"Ninadhani haitoshi kuishia kumpongeza mtu aliyejifungua mapacha, badala yake yatazamwe mazingira aliyomo na vikwazo anavyopitia katika kuhudumia watoto hao ili mwisho wake vikwazo hivyo vipatiwe ufumbuzi," anasema.

Diana anataja njia mojawapo ya kutatua vikwazo vinavyowakabili wazazi wa aina hiyo, ni kutafuta uwezekano wa kuingiza kundi hilo katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii kama ambavyo yameingizwa makundi mengine.

"Lakini pia niiombe serikali iangalie uwezekano wa kuwapa bima za afya, kwani kutegemea kuwa watoto wadogo wanatibiwa bure, wengi wao hukosa huduma hiyo kwa kuambiwa hakuna," anasema Diana.

Mwenyekiti huyo anasema anaamini familia zenye mapacha zinazokabiliwa na changamoto mbalimbali nchini ni nyingi ambazo hazijafikiwa, na kwamba taasisi yake ikipata uwezeshwaji itazunguka nchi nzima kuwafuatilia.

"Taasisi yetu inajishughulisha na msaada kwa familia zenye watoto mapacha zisizo na uwezo.Kwa miaka miwili ambayo tumefanya kazi hii tumebaini mengi, ndio maana tunashauri waingizwe katika kundi maalum,"anasema.

Aidha, anasema kwa mara ya kwanza walifanya maadhimisho ya Siku ya Mapacha Novemba 11 mwaka jana, kwa kuwakusanya katika viwanja vya Shirika la Posta Kijitonyama Dar es Salaam.


Mwenyekiti anafafanua kuwa mwaka huu wamesherehekea kivingine kwa kuwatambelea majumbani mwao na kuwapa msaada wa hali na mali wakisaidiana na kundi alilolitaja kwa jina la Twins Care.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutoka enzi ya kuanika betri juani hadi kuchaji

**Na Adam Fungamwango**

● Zingine zilibondwa na kufungwa nyuma ya redio




DUNIA inakwenda kasi sana na usipokwenda nayo inakuacha. Kwa sasa ni nadra sana kuona betri kavu ambazo zilikuwa zinatumika kwenye redio na tochi.

Labda unaweza ukaziona nyingi ni zile saizi ndogo ambazo zinanunuliwa kwa ajili ya kuweka kwenye 'rimoti' za televisheni na 'deki'. Zile kubwa za kuweka kwenye redio kwa sasa hata wenye maduka zimekuwa adimu hasa mijini kwa sababu hata wafanyabiashara hawaziweki sana madukani kwa sababu hazina wateja kama zamani.

Betri zile biashara zake kwa sasa asilimia kubwa ipo vijijini, lakini hata hivyo siyo kama ilivyokuwa zamani kwani hata aina ya redio nyingi kwa sasa hazitumii aina ile ya betri.

Sababu kubwa ya kwanza ni kwamba kwa sasa mijini karibuni nyumba nyingi zina umeme tofauti na zamani, hivyo redio nyingi zinaunganishwa tu kwenye nyaya badala ya kutumia betri kavu.

Halafu kama nilivyosema kuwa kuna mabadiliko makubwa kwenye viwanda vya kutengeneza redio kwani kwa sasa zinazokuwa hazitumiki tena aina ile ya betri za zamani ambazo wazee wa wakati huo waliziita 'mawe', badala yake redio nyingi kama si zote zinatumia betri ambazo huwa pia zinatumika kwenye simu za mkononi.

Ukiwa na betri la simu, unaweza pia ukalitumia kwenye redio pia. Kinachofanyika ni kuchaji tu. Betri linawekwa, chaji ikiisha redio inazimika, mtumiaji anachaji na maisha yanaendelea mpaka betri lenyewe litakapoharibika.

Vilevile kuna aina zingine za redio ambazo zenyewe unachaji tu na kutumia, hazina betri, chaji ikiisha inazimika, unarudia tena kuchaji na kuendelea kusikiliza.

Haya ndiyo maisha ya sasa. Redio za kuchaji tu, tofauti na zamani ambapo ilikuwa ni lazima mtu akanunue betri na kuziweka kwenye redio na zikiisha chaji zinatupwa zinakwenda kununuliwa nyingine.

Na hata hizo betri zilikuwa na saizi. Kuna ndogo sana ambazo ni maalum kwa redio ndogo, halafu za kati na zile kubwa na hutumika kulingana na ukubwa na redio yenyewe.

Hata hivyo kutokana na maisha magumu, ukosefu wa pesa, kubana matumizi au kujiongeza, zamani watu wengi hawakuridhika betri zikiisha chaji basi azitupe tu akanunue zingine. Ni mpaka ahakikishe hazina tena uwezo wa kufanya chochote.

Ndiyo maana wakati huo betri zikiisha chaji walikuwa wakizianika juani. Kulikuwa na staili kadhaa ya kuanika betri kavu. Kwanza kabisa zilikuwa zinawekwa juu ya bati. Wengine waliziweka dirishani. Wote hawa lengo lilikuwa moja ni kuchaji. Yaani walifanya kama wanavyofanya sasa wanavyochaji betri hizi za kisasa kwenye umeme. Lakini hii haikuwa rasmi, ila wao wenyewe tu walijiongeza, kiuhalisia zikiisha zilitakiwa zitupwe.




Kuna waliokuwa wakizibondabonda kwa lengo tu la kujaribu kurudisha ile nguvu ya chaji ya awali. Zilibondwa hadi kupoteza umbile lake la kawaida kama betri.

Hali ikizidi kuwa mbaya, wengine sasa hawaziweki ndani. Kuna redio ziliingiza betri mbili, nne, sita mpaka nane. Chaji zikiisha kwenye betri, wapo waliobuni kukusanya betri nyingi zaidi ya zilivyopendekezwa, wanazifunga na waya nje.

Waya inaanza kufungwa ndani sehemu ambazo zinaunganishwa betri, halafu inatolewa nje. Zinafungwa kwenye idadi kubwa ya betri ambazo haziwezi kuingia zote ndani kwa sababu ni nyingi kuliko inavyotakiwa zinaunganishwa kwa pamoja na kufungwa na mipira ya manati.

Zinaweza kuunganishwa hata betri kumi, lakini chaji yake inakuwa kama ya betri nne tu, lakini kwa sababu idadi hiyo ni kubwa, basi zinakuwa zimefungwa nje ya redio.

Kali kuliko yote kuna waliokuwa wanapeleka betri hizi msalani, kwa sababu kulikuwa na dhana kuwa kule chaji yake inakuwa kubwa zaidi na haiishi upesi.

Pamoja na yote hayo, hakukuwa na uthibitisho wenye ushahidi wa kitaalam ulioonyesha kama ni kweli ukifanya yote hayo, betri zinarudi kwenye hali yake ya kawaida na kuwa kama mpya, au kama zimechajiwa.

Kilichokuwa kikionekana ni kwamba yakifanyika yote hayo, betri zinarudi na nguvu mpya hata kama redio ilikuwa hailii itaanza kuzungumza, lakini haitochukua muda wa siku nzima zaidi ya masaa fulani tu, nguvu ya chaji inaisha na zinarudi kuwa vile vile.

Na kazi inaendelea kuwa vile vile zitaanikwa, zitabondwa, zitapelekwa msalani, hadi siku ambayo itapatikana pesa ya kununulia betri mpya.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Watu mil 10 wakosa umeme Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amesema raia wake milioni 10 hawana umeme baada ya mashambulizi mapya ya makombora yaliyofanywa na Russia jana.

Katika mashambulizi hayo, watu saba waliuawa, huku idadi zaidi ya vifo ikitarajiwa kuongezeka.

"Tunafanya kila kitu kurekebisha usambazaji," alisema Zelensky alisema katika hotuba yake ya jana usiku.

Aliongeza kwamba mfumo wa ulinzi wa anga ulifanikiwa kudungua makombora sita na ndege zisizo na rubani tano.

Usiku wa kuamkia Ijumaa, Russia iliishambulia Ukraine kwa makombora na kuharibu mitambo zaidi ya nishati ya umeme na majengo mengine ya kiraia kwa siku mbili.

Mashambilizi hayo yanaelezwa kuwa makali zaidi ya mabomu kutokea tangu kuanza kwa vita hivyo.

Watu saba walikufa wakati kombora lilipogonga kizuizi cha ghorofa huko Vilnyansk, karibu na mji wa kusini wa Zaporizhzhia, ofisi ya rais wa Ukraine ilisema.

Kiwanda cha kuzalisha gesi mashariki na kiwanda cha makombora huko Dnipro vilikuwa miongoni mwa malengo ya mashambulizi hayo.

Watu wanaokabiliwa na ukosefu wa umeme wako hasa Kyiv, mji wa magharibi wa Vinnytsia, Odesa na Sumy ulioko kaskazini-mashariki.

Zelensky aliishutumu Russia kwa kuharibu usambazaji wa umeme na gesi kwa watu wake.

Kiongozi wa Ukraine alirudia wito wake kwa washirika kutoa ulinzi kamili wa anga kwa nchi yake, akisema kuwa kufanya hivyo kutaifanya Russia kumaliza vita.

Hata hivyo Russia imehalalisha mashambulizi yake ya hivi karibuni kwa kuishutumu Ukraine kutokuwa na nia ya mazungumzo.

Wakati huo huo, kampuni ya nishati inayomilikiwa na serikali ya Naftogaz ilisema mitambo yake ya kuzalisha gesi mashariki mwa Ukraine imekumbwa na shambulio kubwa.

Papa kupatanisha

Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis amesema kwamba Vatican iko tayari kuwa mpatanishi kwenye mazungumzo yatakayowezesha kumaliza vita kati ya Russia na Ukraine.

Papa Francis amerejea matamshi hayo wakati wa mahojiano na gazeti la kila siku la nchini Italia la La Stampa ambapo amesema mazungumzo ya dhati kati ya pande hasimu ndiyo yataleta amani ya kweli baina ya nchi hizo.

Alisema msingi wa majadiliano ni lazima kwanza pande zote mbili zisafishe mioyo na kuwa tayari kwa mazungumzo na kisha kuweka chini silaha.

Matamshi yake yanatolewa wakati mapambano bado yanaendelea nchini Ukraine ambapo jana Russia ilisema inaimarisha vikosi vyake kwenye Rasi ya Crimea iliyoinyakua kutoka Ukraine mwaka 2014.

Hatua hiyo inatokana na vikosi vya Ukraine kulikamata jimbo jirani la Kherson. **DW**



Wakazi wa mji wa Kherson wakipokea msaada wa chakula baada ya eneo hilo kurudishwa na Russia hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

## Uganda kupeleka wanajeshi 1000 DRC

**KAMPALA,** UGANDA

UGANDA imetangaza itatuma wanajeshi wake 1000 katika ujumbe wa kulinda amani katika eneo la Ituri nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Vikosi vya Uganda viko ndani ya DRC vikijishughulisha kivyake katika misheni ya kivita pamoja na vikosi vya serikali dhidi ya Allied Democratic Forces (ADF) ambalo ni kundi la waasi wa Uganda lenye kambi nchini humo.

Msemaji wa Jeshi, Jenerali Felix Kulaigye aliambia BBC kwamba wanajeshi hao wamekuwa mafunzoni tangu Juni katika wilaya ya Kiruhura, magharibi mwa Uganda.

Tangazo hilo linakuja siku chache baada ya nchi jirani ya Kenya kutuma kundi la pili la wanajeshi wake katika jimbo la Kivu Kaskazini nchini DRC, kushiriki katika ujumbe wa kulinda amani wa kikanda uliokubaliwa mwezi Aprili na nchi saba za Afrika Mashariki ambazo DRC ni mwanachama wake.

Waasi wa M23 katika wiki za hivi karibuni wameendelea kusonga mbele kuelekea Goma, mji mkuu wa Kivu Kaskazini huku wakielekea kuteka maeneo zaidi.

Maelfu ya watu wamekimbia makazi yao.

Viongozi wa Afrika Mashariki walitangaza kuwa mazungumzo yanayolenga kuleta amani mashariki mwa DRC yatafanyika nchini Kenya mwishoni mwa mwezi huu. **BBC**

## Korea Kaskazidi yazidisha hofu, yajaribu kombora jipya la ICBM

**SEOUL,** KOREA KUSINI

KOREA Kaskazini imerusha kombora linaloshukiwa kuwa la masafa marefu.

Taarifa iliyotolewa na Korea Kusini, ilisema kombora hilo aina ya ICBM lilirushwa karibu na mji mkuu wa Korea Kaskazini Pyongyang.

Hata hivyo, Japan ilisema kuwa kombora hilo lilitua kwenye maji magharibi mwa kisiwa chake cha kaskazini cha Hokkaido.

Waziri mkuu wa Japan Fumio Kishida alisema inaaminika kuwa lilitua takriban kilomita 200 magharibi mwa kisiwa ambacho kipo karibu na kisiwa chake ndani ya eneo la kiuchumi la Japan.

Aliongeza kuwa hakuna ripoti za awali za uharibifu wa meli au ndege.

"Kwa kawaida tulifanya maandamano makali dhidi ya Korea Kaskazini, ambayo imerudia uchochezi wake mara kwa mara," alisema Kishida wakati akiwaambia waandishi wa habari nchini Thailand.

Siku ya Alhamisi Waziri wa Mambo ya Nje wa Korea Kaskazini Choe Son Hui, alionya kuhusu jibu kali kwa mipango ya Marekani ya kuimarisha uwepo wake katika kanda hiyo.

Pia ilirusha kombora la masafa mafupi ya balestiki siku hiyo hiyo.

Rais wa Marekani Joe Biden, kiongozi wa Korea Kusini Yoon Suk-yeol na Waziri Mkuu wa Japan Fumio Kishida walikuwa wakijadili hali hiyo kando ya mkutano wa kilele cha nchi za Asia nchini Cambodia.

Biden baadaye alisema washirika hao watatu walemingana zaidi kuliko hapo awali juu ya tabia ya uchochezi ya Korea Kaskazini .

Mshauri wake wa usalama wa kitaifa aliapa kutoa jibu la umoja ikiwa Korea Kaskazini itafanya jaribio la saba la silaha za nyuklia, ambalo idara za kijasusi za Marekani na Korea Kusini wamekuwa wakionya kwa miezi kadhaa.

Aliongeza kuwa hakuna ripoti za awali za uharibifu wa meli au ndege.

"Kwa kawaida tulifanya maandamano makali dhidi ya Korea Kaskazini, ambayo imerudia uchochezi wake mara kwa mara, Kishida aliwaambia waandishi wa habari nchini Thailand.

Korea Kaskazini imefanyia majaribio mengi ya makombora mwaka huu, huku hali ya wasiwasi ikiongezeka.

Uzinduzi wa mpango wa makombora ya ICBM umekuwa mtihani wa nane kwa mwaka huu. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**WILLIAM ITUNGI MDACHI** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha chuo cha DIPLOMA IN ACCOUNTANCY chenye usajili namba **OD.004305D1.2008** kilichotolewa na COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION mwaka 2010, cheti cha chuo cha BACHELOR DEGREE IN ACCOUNTANCY chenye usajili namba **TIA/DSM/BAC/2010/2011/131** kilichotolewa na TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY mwaka 2013 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0345-0291** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia USAGARA SECONDARY SCHOOL mwaka 2003. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochopte cha polisi.

POLISI TAARIFA: **URP/IR/353/2015**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA YASSIN** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE HJ1258EX** yenye usajili namba **MC 440 CTD ,** CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK27L0099149.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SO/RB/1036/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ATHUMANI JUMA MAGANGA**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye namba za usajili **(T373 BSM),** Pamoja na leseni ya udereva yenye namba **(NO.4001203593),** pamoja na kadi ya bank NMB account namba **(23210027736).** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu au piga simu no:**0754508070.**

**MOR/MOR/RB/446024/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.160 of 2022**

**In the matter of the Estate of the late WILLIAM MACHAKA HAMASI**
**Of Mnase Chamwino within Dodoma Region**

**AND**

**In the matter of an application for letters of administration by KELOSI WILLIAM MACHAKA.**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **22 Day of 11, 2022**

**Dated at Dodoma this 3rd day of November,2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri la Ndoa Na 45/2022**

**Jina la mdai: MARGRETH JULIUS**

**Jina la mdaiwa: JAMES MICHAEL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: JAMES MICHAEL WA NYANKUMBU**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:**YA TALAKA NA MGAWANYO WA MALI** Kwa hiyo unatakiwa Kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 24/11/2022 saa 08:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10/11/2022

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-6

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Mshtuko wa moyo kwa mbali ukampiga Adel. Kama mwanaume, pamoja na kwamba alijua msichana kama yule hawezi kukosa mwanaume, lakini wivu ulimshika ghafla.

"Mpenzi au mchumba?"

"Mchumba." Lilikuwa jibu baya zaidi kuliko la mwanzo.

"Amekutolea barua nyumbani kwenu?"

"Nd...iy...o" Akajibu kwa unyonge zaidi.

Ni kama msichana huyo hakutaka kumuumiza Adel. Lakini akalazimika kumwambia ili baadaye usitokee mtafaruku.

"Anaitwa nani?" Lilikuwa swali lisilokuwa na maana yoyote ile, lakini lilimtoka kwa wivu na hasira iliyojificha."

Hata kama akijua jina ingemsaidia nini? Hata yeye mwenyewe alitambua kuwa swali lake halikuwa na maana yoyote.

"Enock." Akajibiwa.

"Yupo hapa hapa kijijini?"

"Ndiyo na ndiyo maana jana nilikwambia usije nyumbani kwa sababu huwa anakuja mara kwa mara na watu wote kijijini wanafahamu hilo. Hapa yenyewe kama akitokea mtu akatuona na kwenda kumwambia itakuwa kasheshe, ndiyo maana mimi jana nilitaka kuja kwa siri, na hapa nimejiiba tu."

Majibu hayo yote yalimfanya Adel kushusha pumzi ndefu na kuwa mpole ghafla hali ambayo hata Mary hakupata shida kuitambua.

"Pole sana Adel, hata mimi naona hali unayoipata baada ya kukwambia hivyo, ndiyo maana mimi sikutaka kukwambia, nilijua tu haya, utahuzunika na kusikitika, wewe ni shujaa wangu ujue."

"Mary, nikwambie kitu, kama ungeuona moyo wangu umeumia na kuvunjika sana. Ukweli tu ni kwamba nilitokea kukupenda ghafla kutoka ndani kabisa ya moyo wangu. Naheshimu maamuzi yako. Naheshimu muda, ni kwamba kuna mtu amewahi mimi nilichelewa, lakini nikwambie tu, nakupenda sana na nitaendelea kukupenda." Wakati anaongea maneno hayo machozi yalianza kumtoka Adel. Mwanamke hakuvumilia. Akatoa khanga aliyojitanda na kuanza kumfuta machozi.

"Usilie Adel, nimekubali na nimeamini kuwa unanipenda kutoka ndani ya moyo wako. Pamoja na kupendwa na wanaume wengi, lakini hakuna hata mmoja aliyewahi kulia au kutokwa machozi kwa ajili yangu. Umesema utaheshimu maamuzi yangu, nimefurahi sana kwa hilo, pia umesema utaendelea kunipenda. Na mimi nakwambia wewe si mpenzi wangu wa mwili, lakini utakuwa mpenzi wangu kwenye moyo wangu." Wakati akiongea maneno hayo, huku akiendelea kumfuta machozi walisikia kuna mtu anawakaribia.




**"Sasa mbona watu wangu wa upelelezi wanasema yule kijana mpya kijijini kwetu ni mpenzi wake?"**

Wote walishtuka na kugeuka kuangalia kuna nini. Hakuna binadamu bali ni mbwa aliyekuwa anakatiza njia. Wote waliangaliana tena na kutabasamu.

"Mary, sijui niseme nini. Mimi nimetoka mjini, Dar es Salaam, ambapo kuna kina aina ya mwanamke aliyeitwa au kujiita mrembo. Wanawake wenye uzuri wa asili, na wenye kujipamba wakapambika, lakini sijaona yoyote mzuri kushinda wewe. Inawezekana wapo, lakini macho yangu mimi na akili yangu imeona kwako. Hata kama kuna Enock, nitaendelea kukupenda daima."

Baada ya kulizana hapo, waliachana. Mary alirejea nyumbani kwao, Adel yeye alivunga kama anakwenda mbele, lakini baadaye alirejea na kupita pale pale nyumbani kwa kina Mary.

Wakati huu sasa yeye alikaa alisimama mlangoni na kumtazama mgeni wake akiwa anapita kwa mbali. Akampungia mkono kwa tahadhari, Adel akatabasamu, naye akarudisha kwa umakini. Ni kama vile alikuwa ananyoosha mkono juu, lakini ndiyo alikuwa anajibu.

************************************

"Mzee Chale mimi nimekwita hapa kuna kitu nataka kukwambia." Akaongea kwa hasira kidogo hali iliyomshangaza Mwenyekiti wa Kijiji.

"Nini tena mwekezaji wetu?"

"Wewe si unasema yule binti ana mchumba wake anaitwa Enock, si ndiyo?"

"Sahihi kabisa."

"Sasa mbona watu wangu wa upelelezi wanasema yule kijana mpya kijijini kwetu ni mpenzi wake?"

"Una uhakika na unachokisema au wanachokwambia watu wako?"

"Ndiyo walivyoniambia, kuwa yule kijana ambaye amekuja hapa kijiji kama wiki mbili zilizopita anaonekana na Mary maeneo ambayo ni tata na yanatia mashaka kuwa huenda wana mahusiano."

"Sasa bwana mwekezaji wewe ulitaka kusemaje?"

"Yule binti si alinikataa mimi, akasema ana mchumba wake, wewe mwenyewe ukasema nisimfuate mchumba wa watu itakuwa ni mbaya, mbona kaja mtu mwingine tena mgeni tu, anamfuata?"

"Kwanza bwana Mosha Usonzo ukae ukijua kuwa penzi halilazimishwi. Ukijua hilo tu kwanza utapunguza hasira zako. Mimi nadhani wa kuona wivu alikuwa ni mchumba wake Enock na siyo wewe. Halafu nikwambie kitu kimoja, siyo ukiona mwanamke anazungumza tu na mwanaume basi wana uhusiano wa kimapenzi, hebu waambie hao wapelelezi wako waendelee kupeleleza. Kama hadi leo Enock hajashtuka au kusema lolote, sidhani kama ni mpenzi wake.

Inawezekana ikawa hata ni kweli yule kijana anamhitaji ndiyo maana walikutana, lakini binti akakataa vile vile."

"Tatizo na wewe ni mwanasiasa sana."

"Ndiyo kazi yangu, ndiyo maana nimewashawishi hata wananchi wamekubali kuuza asilimia kubwa ya ardhi yao." Mzee Chale alimpasha Usonzo huku ikionekana ile jazba yake imepungua.

"Lakini mimi yule mtoto yule?"

"Yupi?"

"Kale kabinti, unajua kazuri sana, kaenda kukubali watu hawana hata mpango..."

"Nani sasa hana mpango, Enock au yule mgeni?"

"Wote wawili." Akajibu na kumfanya mwenyekiti aangue kicheko.

************************************

"Adel huyu ndiyo mchumba wangu ambaye tunatarajia kuwa tutaoana Mungu akipenda."

"Vizuri sana." Akajibu huku akimsogelea na kumpa mkono.

"Mpenzi Enock, huyu ni yule mgeni niliyekuambia kuwa aliniokoa kwenye ajali ya bodaboda siku ile, anaitwa Adel...Adel nani vile..."

"Adel Adam." Mwenyewe akajibu huku bado mikono yake ikiwa imeshikana na ya Enock.

"Ooh, vizuri ahsante sana kwa msaada wako, wewe umehamia kwenye kijiji hiki?"

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MAYELE AELEZEA 'HAT-TRICK', KIBWANA AKICHEKELEA BAO

**Adam Fungamwamngo na Saada Akida**

WAKATI straika wa Yanga, Fiston Mayele, akizungumzia hat-trick aliyofunga katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Big Stars na ukame alioupata hivi karibuni, beki, Kibwana Shomari ameonyesha furaha kubwa baada ya kufunga bao la kwanza tangu ajiunge na timu hiyo mwaka 2020, akitokea Mtibwa Sugar.

Yanga ilimaliza mechi hiyo kwa ushindi wa mabao 4-1, Meddie Kagere, mshambuliaji wa zamani wa Simba akifunga bao pekee la Singida Big Stars katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, juzi usiku.

Mayele aliliambia gazeti hili amefurahi kufunga 'hat-trick' yake ya kwanza katika Ligi Kuu Tanzania Bara, huku akitoa ufafanuzi kwa jinsi alivyoshangilia bao la kwanza.

"Bao la kwanza ni kwa ajili ya mtoto wangu, nimepata mtoto, kama mliona mechi dhidi ya Zalan FC nilifunga nikaweka mpira tumboni, leo (juzi), nimefanya staili tofauti ya ushangiliaji wa kulea kwa ajili ya mtoto wangu aliyezaliwa.

Nimeshukuru sana nimefunga 'hat-trick' yangu ya kwanza kwenye Ligi Kuu na 'nilimisi' sana kufunga, watu wakawa wanasema Mayele hajatetema mwezi mzima, lakini leo (juzi), nimetetema tena," alisema Mayele.

Aliongeza kitendo cha ukame wa kufunga alichokuwa nacho kilimtesa sana na hat- trick yake ya kwanza aliyopata tangu amekuja Tanzania inamjengea imani ya kuendelea kufanya vizuri na kusaidia timu yake kufikia malengo.

"Nimejisikia furaha kufunga Hat trick yangu ya kwanza tangu nimekuja Tanzania kucheza, sababu ya kutoshangilia kwa kutetea bao la kwanza ilikuwa zawadi kwa mtoto wake mpya (kike) ambaye hivi karibuni mke wake amejifungua," alisema Mayele.

Alisema wanasahau matokeo ya mchezo na Singida Big Stars, sasa wanajiandaa kwa ajili ya mechi ijayo watakaocheza ugenini dhidi ya Dodoma jiji FC ambapo wanahitaji kupata pointi muhimu.

Tangu alipofunga bao katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa Septemba 13, mwaka huu ambapo Yanga ilishinda mabao 3-0, Mkongomani huyo alikuwa hajafunga tena licha ya timu yake kupata ushindi kwenye mechi tatu ilizocheza na sare moja.

Straika huyo amefikisha jumla ya mabao sita ambapo sasa anachuana na Moses Phiri wa Simba, Reliants Lusajo (Namungo na Idris Mbombo wa Azam FC, lakini juu yao akiwa Sixtus Sabilo wa Mbeya City ambaye mpaka sasa ndiye kinara katika orodha ya wafungaji akiwa amefunga magoli saba.

**Naye Shomari alisema amefurahi kufunga bao la kwanza tangu aji unge na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

" Hili ndilo goli langu la kwanza, nilikuwa na nia kabisa ya kufunga leo (juzi) na nikafunga, nimefurahi sana," alisema beki huyo.

Yanga wanaondoka jijini kesho kuelekea Singida kwa ajili ya kukabiliana na Dodoma Jiji FC ambao wanatumia Uwanja wa Liti, katika mechi itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni ifikapo Novemba 22, mwaka huu.



Mshindi wa kwanza wa bodaboda katika Kampeni ya Mastabata – Kotekote ya Benki ya NMB, Asumwisye Mwajeka akiijaribu pikipiki baada ya kukabidhiwa katika Tawi la Mkwawa, Iringa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yakabidhi pikipiki na fedha

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

BENKI ya NMB imepata mshindi wa pili wa bodaboda, Charles Mbwilo kutoka Songea mkoani Ruvuma kupitia droo ya shindano la NMB MastaBata Kote-kote.

Katika kampeni hiyo jumla ya Sh. milioni 350 zitatolewa kwa washindi 854 ikiwa ni pamoja na zawadi za pikipiki na safari ya Dubai kwa washindi saba pamoja na wenza wao. Tayari Sh. milioni 15 zimetolewa kwa washindi 150 mpaka sasa na bodaboda mbili zikiwa na thamani ya Sh. milioni sita.

Akizindua droo ya pili ya mchezo huo katika Tawi la NMB - Mkwawa mkoani Iringa, Kaimu Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Manyilizu Masanja alisema lengo ni kuhamasisha matumizi ya NMB Master Card na Master Card QR kwa wateja wake.

Masanja alisema wateja wakifanya miamala yao kupitia kadi ya NMB Master Card au Master Card QR, watakuwa wamejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya ushindi katika droo zijazo.

"Kila unapofanya muamala unajiweka kwenye nafasi nzuri ya ushindi na kuibuka na zawadi," alisema Masanja.

Meneja Mwandamizi Idara ya Kadi, Manfred Kayala aliwahimiza wateja kuendelea kutumia njia hiyo kufanya miamala ili waingie kwenye droo hiyo na baadaye kushinda.

Mshindi wa bodaboda wa wiki iliyopita, Asumwisye Mwajeka baada ya kukabidhiwa zawadi yake, alisema ushindi huo umempa nguvu ya kuendelea kutumia NMB MasterCard kama njia ya malipo.

"Niwahamasishe vijana wenzangu msitembee na fedha mikononi au mifukoni, faida yake mimi nimeona. Nimefurahi kupata bodaboda," alisema.

## Mamilioni ya 10bet sasa yatua Singida

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Simba na Liverpool ya England, Richard Mkumbo kutoka mkoani Singida ameshinda zawadi ya Sh. milioni 11 kupitia jackpot ya katikati ya wiki ya Kampuni ya 10bet ya hapa nchini, imefahamika.

Mkumbo ambaye ameshakabidhiwa kitita hicho alibashiri kwa usahihi mechi 10 za ligi mbalimbali duniani kwa kutumia Sh. 500 tu.

Ushindi huo unamfanya Mkumbo kuwa mshindi wa kwanza wa jackpot hiyo hapa nchini na kukakabidhiwa zawadi yake na Meneja Masoko wa kampuni hiyo, George Abdulrahman katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika jana.

"Mimi ni mjasiriamali na nimekuwa nikibashiri na 10bet mara kadhaa na sikushinda. Hata hivyo sikukata tamaa na kuendelea na kufanikiwa kushinda milioni 11 kwa Sh. 500 tu," alisema Mkumbo.

Kwa upande wake Meneja Masoko wa 10bet Tanzania, George Abdulrahman, alisema wanajisikia fahari sana kubadilisha maisha ya Watanzania kupitia michezo yao ya kubashiri.

## Jamhuri yajipanga kuimaliza Kipanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI cha Jamhuri SC kutoka Pemba kimetamba kitaibuka na pointi tatu katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Kipanga itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Jamhuri, Juma Abdullah, alisema matarajio yake makubwa ni kuvuna alama tatu muhimu katika kila mchezo atakaocheza kwenye uwanja wa ugenini.

Abdullah alisema kuelekea mchezo huo anajua vyema watakutana na timu ngumu yenye wachezaji wazoefu katika ligi hiyo lakini wao pia wamejipanga vyema kuhakikisha wanafanya vizuri.

Kocha huyo alisema kikosi chake kina ari kubwa ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo mitatu iliyobakia katika mzunguko wa kwanza ambayo watacheza ugenini.

"Tumekuja kusaka alama katika michezo yetu mitatu ambayo tutamaliza mzunguko huu wa kwanza tukiwa ugenini, kama unavyojua michezo ya ugenini inakuwa migumu kwa sababu mwenyeji wanataka kutumia uwanja wao vizuri na sisi tumejipanga kukabiliana na hilo ili tupate matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL huenda ikamsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund, Januari. (***Football Insider***)

### MOUNT ASAKWA ENGLAND

LIVERPOOL na Juventus zinafuatilia mazungumzo ya mkataba mpya yanayoendelea kati ya kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 23 na Chelsea. (***Guardian***)

### MOUNT KUIBEBA CHELSEA

CHELSEA inamwona, Mason Mount kama nahodha wa siku zijazo wa klabu hiyo, lakini mkataba wake wa sasa unamfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara wa chini zaidi kwenye kikosi hicho. (***Mail***)

### POCHETTINO KUFUNGUKA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Southampton na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino amesema "atakuwa wazi kwa kila kitu" alipoulizwa kama angependa kuwa kocha wa England. (***Athletic***)

### SOARES AGEUKA LULU

KLABU za Fulham, Bayer Leverkusen na Villarreal zina nia ya kumsajili beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cedric Soares mwenye umri wa miaka 31 kutoka Arsenal, ifikapo Januari. (***ESPN***)

### VILLA ILIMKATAA PALHINHA

ASTON Villa ilikataa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kujiunga na Fulham. (***Football Insider***)

### SUAREZ AIKATAA GREMIO

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Barcelona na Liverpool, Luis Suarez, mwenye umri wa miaka 35 amekataa ofa ya kujiunga na Gremio ya Brazil mara tu mkataba wake na Nacional ya nchini kwao Uruguay utakapokamilika. (***Fabrizio Romano***)

### POLAND ULINZI MKALI

TIMU ya Taifa ya Poland ilisindikizwa na ndege za kivita kuelekea Qatar kwa ajili ya michuano ya Kombe la Dunia. (***Sky Sports***)


### ARGENTINA WABEBA NYAMA

ARGENTINA NA na Uruguay kila moja imechukua kilo 900 za nyama hadi Qatar ili wachezaji na wafanyakazi waweze kula chakula cha nyumbani wakati wa fainali za Kombe la Dunia. (***ESPN***)

### QATAR YAKATAA POMBE

RAIS wa Qatar analitaka Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kubatilisha uamuzi wa kuruhusu pombe kuuzwa katika viwanja vyote vitakavyoandaa mechi za Kombe la Dunia. (***Times***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RASMI MANE NJE KOMBE LA DUNIA

**Ni baada ya mshambuliaji huyo kufanyiwa upasuaji juzi na hivyo...**

**MUNICH,** Ujerumani

SHIRIKISHO la Soka la Senegal limesema, Sadio Mane 30, atakosa "michezo yao ya kwanza" katika mashindano hayo, kwani uchunguzi zaidi wa MRI ulikamilishwa juzi ambapo mshambuliaji huyo alilazimika kufanyiwa upasuaji.

Mane alilazimika kutolewa nje wakati Bayern Munich iliposhinda kwenye Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, dhidi ya Werder Bremen, katika mechi iliyochezwa Novemba 8, mwaka huu.

Bayern Munich wamethibitisha mchezaji huyo "alifanyiwa upasuaji wa mafanikio" siku ya Alhamisi, ili kuunganisha mshipa kwenye eneo la goti.

**"Mshambuliaji huyo ataanza matibabu yake mjini Munich siku chache zijazo," klabu hiyo iliongeza.**

Senegal inaanza michuano ya Kombe la Dunia dhidi ya Uholanzi hapo keshokutwa, wakiwa katika Kundi A na mechi inayofuata watakabiliana na wenyeji Qatar ifikapo Novemba 25, mwaka huu na watamaliza hatua ya makundi kwa kuvaana na Ecuador hapo Novemba 29, mwaka huu.

Mchezaji Bora wa Mwaka wa Afrika mara mbili, Mane ndiye kinara wa kupachika mabao kwa Senegal, baada ya kufunga penalti ya ushindi wakati Simba wa Teranga hao walipoibuka mabingwa wa Fainali za Kombe la Afrika (AFCON) kwa mara ya kwanza Februari, mwaka huu wakiwafunga Misri katika mechi ya fainali.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,051,2
MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
SIMBA
1 | 6.00
X | 3.35
2 | 1.65
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO AFICHUA KUIKATAA SAUDI ARABIA

**DOHA, Qatar**

CRISTIANO Ronaldo amethibitisha alikataa ofa ya fedha nyingi kwenda Saudi Arabia kwa sababu hakuwa na nia kuondoka Manchester United wakati huo.

Ronaldo alipewa ofa ya kuhamia Saudi Arabia kwa euro milioni 350 msimu wa joto lakini alikataa nafasi hiyo, badala yake akachagua kubaki Old Trafford ili kujaribu kuendeleza kiwango chake.

Hata hivyo, amegombana na Kocha, Erik ten Hag, ambaye amekiri hamheshimu, na sasa kuondoka Januari kunaonekana kuwa wazi.

Alipoulizwa kuthibitisha ripoti za ofa kutoka Saudi Arabia, Ronaldo aliiambia Talk TV: “Ni kweli.

“Vyombo vya habari vinasema hakuna mtu anayenitaka, jambo ambalo si sawa. Wanaendelea kurudia ‘hakuna anayemtaka Cristiano’. Je, hakuna mtu atakayetaka mchezaji aliyefunga mabao 32 msimu uliopita?

“Na nilifurahi hapa kusema ukweli, nilihamasishwa kufanya msimu mzuri hapa.

“Ni ngumu. Lakini kwa njia hiyo hiyo, nilifikiri nilikuwa na furaha sana hapa, bado nina uwezo wa kufunga mabao.

“Bado ninaamini naweza kufunga mabao mengi, mengi na kuisaidia timu kwa sababu ninaamini niko vizuri na nina uwezo wa kuisaidia Timu ya Taifa na hata Manchester United.”




# Rabiot: Sikutaka kutua United

**DOHA, Qatar**

KIUNGO wa Juventus ambaye ni raia wa Ufaransa, Adrien Rabiot, amefunguka juu ya dili lake na Manchester United kuvunjika katika dirisha lililopita la majira ya joto.

Wakati dirisha kubwa likikaribia kufungwa, Manchester United ilikua ikuhusishwa kwa karibu sana kumhitaji Rabiot baada ya dili la kiungo wa Barcelona, Frenkie De jong kuonekana limeshindikana.

Baada ya dili hili kushindikana ndipo klabu hiyo ilipoamua kumsajili kiungo kutoka Real Madrid, Carlos Casemiro, ambaye alinunulia kwa kiasi cha paundi milioni 70.

Dili la Rabiot kuonekana limekufa ndipo kiungo huyo ameweza kufunguka namna ambavyo mchakato wake ulivyozimika.

“Ni kweli nilikua nikitajika na Manchester United na nilikua na nafasi ya kupata changamoto ya Ligi Kuu England, lakini chaguo langu la kwanza ilikua ni kubaki ndani ya Juventus.”

Rabiot ambaye amewahi kutamba na PSG ya Ufaransa kwa sasa amekua ni miongoni mwa wachezaji muhimu ndani ya Juventus kutokana na mchango wake mkubwa.



07,683/-

# KAPUYA AWAFUNDA SIMBA QUEENS, KOCHA AFUNGUKA

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa Simba Queens wamepongezwa kwa kupeperusha vyema bendera ya Tanzania na wametakiwa kujipanga upya kwa ajili ya kutafuta tiketi ya kushiriki tena katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake ya msimu ujao.

Hayo yalisemwa na mgeni rasmi, Profesa Juma Kapuya, katika hafla maalumu ya kuwapongeza iliyofanyika juzi usiku kwenye Mgahawa wa Akemi, jijini Dar es Salaam.

Simba Queens ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake ambapo wenyeji, ASFAR FC ya Morocco ilitwaa taji hilo mbele ya Mamelodi Sundowns Ladies kutoka Afrika Kusini.

Kapuya aliwaambia wachezaji wa timu hiyo kuendelea kupambana na kuhakikisha 'moto' waliouwasha katika mashindano hayo ya Afrika hauzimiki.

"Napenda nimpongeze Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, kama mwanamke ameweza kuiongoza vyema klabu, Simba Queens mmeuwasha moto, hakikisheni hauzimiki, uwe kama moto wa Mwenge," alisema Kapuya.

Aliwaambia heshima ambayo wameiweka katika mashindano ya Afrika mwaka huu ni kubwa na hivyo, wanatakiwa kujituma zaidi kuanzia kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania na baadaye CECAFA ili kurejea mwakani kwenye fainali za Afrika wakiwa imara zaidi.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, aliupongeza uongozi wa Wekundu wa Msimbazi kwa kumpa sapoti na hatimaye kutimiza malengo ya klabu kwenye mashindano hayo yaliyokuwa yanasimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Lukula alisema kazi yake ilikuwa rahisi kwa sababu walifanya maandalizi mazuri na baada ya kujifunza mambo mbalimbali, anaahidi wataendelea kufanya vyema na hatimaye kutetea mataji mawili wanayoyashikilia.

Aliongeza amewapa wachezaji wake mapumziko ya wiki moja na Novemba 24, mwaka huu watarejea uwanjani kujiandaa na msimu mpya utakaofanyika kuanzia Desemba 6, mwaka huu.



Wachezaji wa Simba Queens wakiwa katika sherehe ya kupongezwa iliyofanyika jijini, Dar es Salaam juzi usiku kufuatia kumaliza katika nafasi ya nne kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yaliyomalizika Jumapili iliyopita nchini Morocco. **PICHA: SIMBA SC**

## Nabi hesabu kali mashindano CAF

INATOKA UK. 32

tia kuumia kwa Mayele, ingawa anaamini hajaumia sana zaidi ya kusumbuliwa na uchovu kwa kucheza mechi nyingi.

"Kuhusu kiwango cha Joyce Lomalisa, ni mchezaji mzuri na sasa anaanza kuzoea ligi ya Tanzania pamoja na kujenga muunganiko mzuri, ila ni hatari zaidi katika kushambulia," alisema Nabi. Aliongeza ameamua kumpa nafasi kinda, Clement Mzize, kwa sababu amegundua uwezo wa kijana huyo na alizuia uongozi kumtoa kwa mkopo katika timu nyingine kwa sababu aliamini kiwango chake na siku si nyingi ataisaidia Tanzania.

Naye Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van der Pluijm, alisema kikosi chake kimepokea kichapo hicho kutokana na kukosa bahati.

"Tuliingia na mpango wa kuwashambulia lakini hatukuingia katika mfumo wetu, tumepoteza nafasi nyingi, Yanga wamezitumia walizopata, tumekubali matokeo na tunajiandaa kwa michezo ijayo," alisema Mholanzi huyo. Wakati Singida Big Stars wajiandaa kuikaribisha KMC FC, Yanga itaondoka jijini kesho kuelekea Singida kwa ajili ya kuwakabili Dodoma Jiji FC , katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu utakaopigwa Novemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Liti.

## SIMBA, RUVU

INATOKA UK. 32

li, Kocha wa viungo, Kelvin Ndlomo kutoka Afrika Kusini na mwalimu wa magolikipa, Chlouha Zakaria, raia wa Morocco unatarajiwa kurejesha utimamu wa mwili wa wachezaji wao.

"Tunaamini makipa watakuwa imara zaidi, lakini wachezaji wote watakuwa na wakati mzuri, tutahakikisha kila kitu kinarejea kwenye mstari kwa sababu tuko kwenye mapambano," Ahmed aliongeza.

Alisema pia uongozi wa klabu hiyo unatarajia kumtambulisha kocha mpya wakati wowote kuanzia wiki ijayo huku pia ikimpa baraka kocha wake msaidizi, Selemani Matola, kwenda kuongeza ujuzi katika taaluma hiyo. Wekundu wa Msimbazi watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 ambao waliupata dhidi ya Ihefu katika mchezo wao uliopita, bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa na Mosses Phiri.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/11/22 | 18:00 | Fleetwood Town vs Bolton Wanderers | 3.05 | 3.35 | 2.24 |
| 02. 19/11/22 | 18:00 | Burton Albion vs Plymouth Argyle | 2.65 | 3.40 | 2.50 |
| 03. 19/11/22 | 18:00 | Port Vale vs Charlton Athletic | 2.33 | 3.35 | 2.90 |
| 04. 19/11/22 | 18:00 | Cambridge United vs Accrington Stanley | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 05. 19/11/22 | 18:00 | Colchester United vs Doncaster Rovers | 2.27 | 3.25 | 3.10 |
| 06. 19/11/22 | 18:00 | Grimsby Town vs Stevenage FC | 3.00 | 3.25 | 2.32 |
| 07. 19/11/22 | 18:00 | Cove Rangers FC vs Greenock Morton FC | 2.55 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 19/11/22 | 18:00 | Inverness Caledonian Thistle FC vs Ayr United FC | 2.90 | 3.45 | 2.31 |
| 09. 19/11/22 | 18:00 | Queen of The South FC vs Montrose FC | 2.48 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 19/11/22 | 18:00 | Albion Rovers FC vs Stranraer FC | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 11. 19/11/22 | 18:00 | Annan Athletic FC vs Elgin City FC | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 12. 19/11/22 | 18:15 | SD Ponferradina vs Real Oviedo | 2.55 | 3.05 | 2.85 |
| 13. 19/11/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs CD Leganes | 2.28 | 3.05 | 3.30 |
| 14. 19/11/22 | 22:00 | MVV Maastricht vs Almere City FC | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 15. 20/11/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.80 | 3.30 | 2.45 |
| 16. 20/11/22 | 19:00 | Qatar vs Ecuador | 3.30 | 3.10 | 2.26 |
| 17. 20/11/22 | 21:00 | Racing Santander vs Burgos CF | 2.30 | 2.95 | 3.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 19/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 5351 | Mbeya City vs Geita Gold FC | 2.55 | 2.75 | 3.20 |
| 17:00 | 1494 | Estonia vs Lithuania | 2.87 | 3.06 | 2.35 |
| 17:00 | 1702 | Banik Ostrava vs Sparta Prague | 3.25 | 3.25 | 2.06 |
| 17:00 | 2992 | Latvia vs Iceland | 3.46 | 3.36 | 1.95 |
| 17:00 | 3648 | Ceske Budejovice vs Hradec Kralove | 2.73 | 3.12 | 2.42 |
| 17:30 | 3638 | Cardiff Met Uni. vs Bala Town | 3.01 | 3.40 | 2.11 |
| 17:30 | 3876 | Flint Town United vs Newtown AFC | 2.85 | 3.40 | 2.35 |
| 17:30 | 4808 | FC Volendam vs TEC | 2.32 | 3.46 | 2.63 |
| 18:00 | 1175 | Clyde vs Falkirk FC | 3.96 | 3.61 | 1.80 |
| 18:00 | 1391 | Raith Rovers vs Queens Park | 2.01 | 3.45 | 3.35 |
| 18:00 | 1601 | Peterhead vs Dunfermline | 5.72 | 4.34 | 1.47 |
| 18:00 | 1673 | Bohemians vs Hlucin | 1.18 | 6.25 | 10.74 |
| 18:00 | 1877 | FC Chiasso vs Breitenrain | 1.98 | 3.49 | 3.25 |
| 18:00 | 2094 | Oxford Utd vs Forest Green | 1.50 | 4.15 | 5.74 |
| 18:00 | 2156 | Queen of South vs Montrose | 2.35 | 3.36 | 2.76 |
| 18:00 | 2326 | Barnsley vs MK Dons | 1.80 | 3.43 | 4.28 |
| 18:00 | 2455 | Edinburgh City vs Alloa Athletic | 2.58 | 3.32 | 2.53 |
| 18:00 | 2472 | Cheltenham vs Wycombe | 3.37 | 3.32 | 2.07 |
| 18:00 | 2636 | Sheffield Wed vs Shrewsbury | 1.46 | 4.26 | 6.34 |
| 18:00 | 2761 | Crusaders Belfast vs Newry City AFC | 1.25 | 5.45 | 8.37 |
| 18:00 | 2983 | Inverness vs Ayr United | 2.85 | 3.39 | 2.27 |
| 18:00 | 3303 | Warrenpoint vs Dergview | 1.34 | 4.66 | 7.19 |
| 18:00 | 3345 | Partick Thisle vs Arbroath | 1.90 | 3.49 | 3.69 |
| 18:00 | 3479 | Cove Rangers vs Morton | 2.51 | 3.30 | 2.61 |
| 18:00 | 3548 | Lincoln vs Morecambe | 1.83 | 3.47 | 4.06 |
| 18:00 | 4361 | Carrick Rangers vs Portadown FC | 1.29 | 5.07 | 7.99 |
| 18:00 | 4474 | Burton vs Plymouth | 2.78 | 3.48 | 2.31 |
| 18:00 | 4755 | Cambridge Utd vs Accrington | 2.35 | 3.32 | 2.83 |
| 18:00 | 4811 | Bristol Rovers vs Peterborough | 2.97 | 3.47 | 2.20 |
| 18:00 | 5087 | Glenavon vs Coleraine FC | 2.72 | 3.60 | 2.20 |
| 18:00 | 5811 | Port Vale vs Charlton | 2.37 | 3.28 | 2.83 |
| 18:00 | 5833 | Fleetwood Town vs Bolton | 3.03 | 3.33 | 2.23 |
| 18:15 | 5050 | Ponferradina vs Real Oviedo | 2.48 | 2.98 | 2.93 |
| 18:30 | 5463 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.34 | 3.61 | 2.62 |
| 19:00 | 2167 | Ruvu Shooting vs Simba | 6.00 | 3.35 | 1.65 |
| 19:00 | 5175 | BSC Young Boys vs SC Kriens | 2.62 | 3.50 | 2.31 |
| 19:30 | 5484 | Albania vs Armenia | 1.66 | 3.73 | 5.24 |
| 20:00 | 2416 | Kosovo vs Faroe Islands | 1.69 | 3.69 | 5.06 |
| 20:00 | 5002 | Turkey vs Czech Republic | 2.16 | 3.37 | 3.32 |
| 20:00 | 5881 | FC Aarau vs FC Schaffhausen | 1.77 | 3.89 | 3.60 |
| 20:00 | 5918 | Gibraltar vs Andorra | 3.03 | 3.08 | 2.47 |
| 20:15 | 1882 | Penybont vs The New Saints | 8.40 | 5.40 | 1.30 |
| 20:30 | 5013 | Tenerife vs Huesca | 2.12 | 3.04 | 3.58 |
| 20:30 | 5130 | Sporting Gijon vs Leganes | 2.33 | 2.98 | 3.17 |
| 21:00 | 4938 | Tondela vs GD Estoril | 3.07 | 3.17 | 2.18 |
| 22:00 | 5652 | Maastricht vs Almere City | 2.82 | 3.61 | 2.21 |
| 22:30 | 2579 | Sweden vs Algeria | 1.99 | 3.44 | 3.74 |
| 22:30 | 4894 | Colo Colo vs Betis | 1.83 | 3.69 | 3.55 |
| 23:00 | 3175 | Zaragoza vs Malaga | 2.02 | 2.97 | 4.05 |
| 23:00 | 4483 | NAC Breda vs PEC Zwolle | 3.39 | 3.64 | 1.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Novemba 19, 2022

Nipashe



UKURASA 29

## Rasmi Mane nje Kombe la Dunia



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' (kulia), akimkabidhi nahodha wa Simba Queens, Oppah Clement, tuzo baada ya timu hiyo kutinga hatua ya nusu fainali katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yaliyomalizika Jumapili iliyopita nchini Morocco. Simba Queens ilifanyiwa sherehe maalumu juzi usiku. **PICHA: SIMBA SC**

## Nabi hesabu kali mashindano CAF

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupata ushindi mnono, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema matokeo mazuri waliyopata dhidi ya Singida Big Stars, sio kipimo sahihi kuelekea katika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga iliendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi baada ya kuifunga Singida Big Stars mabao 4-1 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku ambapo Fiston Mayele, alipiga 'hat-trick'.

Mayele kafikisha mabao sita sawa na Moses Phiri wa Simba, Idriss Mbombo (Azam FC) na Reliants Lusajo wa Namungo FC wakati kinara ni mshambuliaji wa Mbeya City, Sixtus Sabilo, ambaye ana magoli saba. Nabi alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi huo mnono ukiwa ni wa kwanza katika msimu huu lakini matokeo hayo hayawezi kuwafanya wajiamini na kuona ana kikosi bora kwa asilimia 100.

Kocha huyo raia wa Tunisia alisema kuna mapungufu ameyaona katika kikosi chake na anatarajia kuyafanyia kazi kwa sababu hajafikia malengo yake ya kuiona Yanga inakuwa moja ya timu bora na tishio hasa wanaposhiriki michuano ya kimataifa.

"Wachezaji wangu wamepambana kwa sababu ya muda wa kujiandaa ulikuwa mchache, kikubwa tuliwaanda kisaikolojia na kuongea nao kwa kuwataka kucheza mechi zote kama fainali.

Matokeo dhidi ya Singida Big Stars hayawezi kutupa kupimo cha kujiona bora kwa sababu tunakwenda kushindana na timu bora zaidi kwenye hatua makundi ya Kombe la Shirikisho, tumeona mapungufu na tunaenda kufanyia kazi," alisema Nabi.

Aliongeza wachezaji wake wanatakiwa kupambana na kufahamu kutetea ubingwa sio kazi nyepesi na anaendelea kuwapongeza kwa kufuata maelekezo aliyowapa mazoezini katika mchezo huo uliopita.

"Mikakati yetu kuelekea mchezo dhidi ya Singida Big Stars kwa asilimia kubwa mipango ilifanikiwa licha ya wachezaji kuwa na uchovu wa safari kutoka Mwanza, lakini niliwapa mapumziko ya kutosha kabla ya mchezo wa leo (juzi), tunashukuru mipango ya mechi imeenda sawa," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa anasubiri taarifa rasmi kutoka kwa daktari wa timu kufua-

INAENDELEA UK. 31

# Simba, Ruvu mechi dume

### ●●●Chama arejea kuongeza nguvu huku Maafande wakitamba...

**Na Saada Akida**

KUREJEA kikosini kwa kiungo Mzambia, Clatous Chama ni moja ya kicheko kwa Wekundu wa Msimbazi wanaotarajia kuvaana na Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 1: 00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Chama pamoja na Stephanie Aziz Ki wa Yanga walifungiwa mechi tatu kwa sababu ya kukataa kusaliamiana wakati timu zao zilipokutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu.

Hata hivyo, Simba itashuka katika mchezo huo wa ugenini ikiendelea kuwakosa wachezaji wake, Nelson Okwa na Peter Banda ambao ni majeruhi huku Jimmyson Mwanuke, John Bocco, Israel Mwenda na Jonas Mkude, wamepona na wanatarajia kuwa sehemu ya kikosi kitakachowakabili Maafande hao kutoka Mlandizi mkoani Pwani.

Kwa upande wa Ruvu Shooting wao watamkosa mshambuliaji wao mkongwe, Abdulrahman Mussa ambaye amekwenda katika kozi ya jeshi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yanakwenda vizuri na jambo muhimu wamejipanga kukutana na timu inayofundishwa na kocha mzuri na mzoefu katika ligi hiyo.

Mgunda alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana katika dakika zote za mechi hiyo ili kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa.

"Mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa, zile nafasi tunazotengeneza tunatarajia tutazitumia vizuri. Hatutakiwi kuingia uwanjani tukiwa na matokeo mfukoni mwetu.

Chama amerudi kundini na adhabu yake imeisha juzi na kesho (leo) atakuwa sehemu ya mchezo kwa sababu tayari ametumikia adhabu yake, mechi itakuwa ya ushindani na tumejiandaa kwa ajili ya kuwakabili wapinzani wetu," alisema Mgunda.

Kocha huyo wa zamani wa Coastal Union, alisema wataingia kucheza mchezo huo kwa kuwaheshimu wapinzani wao kwa sababu anafahamu mbinu za kocha wao ambaye mara kadhaa wachezaji wake huonyesha kiwango kizuri.

"Tutacheza kwa kuwaheshimu sana Ruvu Shooting kwa sababu katika mechi zilizopita hawakupata matokeo mazuri, watakuja kivingine kutafuta matokeo mbele yetu, kulingana na ubora na mapungufu yao tumefanyia kazi ili kutafuta pointi tatu katika mechi hiyo," alisema Mgunda.

Ally Salum, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake wa Simba, alisema wako tayari kuwakabili Ruvu Shooting na kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri ili kufikia malengo yao.

"Benchi la ufundi limeshafanya majukumu yao na kazi kubwa imebaki kwetu sisi kwenda kutafuta matokeo mazuri kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wetu na kuendelea kujikusanyia pointi muhimu na kufikia malengo yetu," alisema golikipa huyo chaguo la tatu la Simba.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohammed, alisema wametoka kwenye uwanja wa mazoezi na sasa wako tayari kukabiliana na Simba.

Mohammed alisema wataingia katika mchezo huo wakiwaheshimu Simba kwa sababu ya kufahamu ubora wao kuanzia katika benchi la ufundi pamoja na wachezaji walioko ndani ya kikosi chao.

"Ligi imekuwa ngumu na kwa sababu hiyo tumejiandaa kupambana na Simba ili kuzipata pointi tatu, ule uteja wetu dhidi ya Wekundu wa Msimbazi mwisho wake ni kesho (leo)," alisema kocha huyo.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Okwa ameomba ruhusa ya wiki moja ya kwenda kwao kwa ajili ya matibabu na mapumziko maalumu.

"Kwa sababu ya majeruhi yake ya muda mrefu, uongozi umempa ruhusa ya wiki moja lakini anatakiwa kuzingatia masharti ya matibabu aliyopewa na jopo la madaktari wa timu," alisema Ahmed.

Aliongeza ujio wa makocha wapya wawi-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >